

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Nane – Tarehe 17 Novemba, 2011

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 2010.

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza maswali kwa Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 38(2), leo Waziri Mkuu hayupo, kwa hiyo, tunaendelea na maswali ya kawaida.

Na. 99

Kukosekana kwa Huduma ya Maji Safi na Salama Tarime

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE aliuliza:-

Tangu enzi za Uhuru hadi sasa Wilaya ya Tarime haijawahi kupata maji safi na salama kwa matumizi ya Wananchi:-

- (a) Je, Serikali haioni kuwa haiwatendei haki Wananchi wa Tarime kwa kutowapatia huduma ya maji safi na salama?
- (b) Je, Serikali ina mkakati gani katika kutatua tatizo hilo haraka iwezekanavyo?
- (c) Je, Serikali inasema nini juu ya ahadi zilizowahi kutolewa za kutatua tatizo la maji Wilaya ya Tarime?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Niinaomba kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika Wilaya ya Tarime ni asilimia 30 kwa maeneo ya Vijiji na asilimia 52 katika maeneo ya Mijini hadi kufikia mwaka 2010. Kwa kuzingatia hali hii, Serikali imejenga tanki kubwa la kuhifadhia maji, ununuzi wa pampu kwa ajili ya kusukuma maji kutoka Bwawa la Togota na kupanua mtando wa maji katika Mji wa Tarime. Juhudi hizi zimewanufaisha Wananchi waishio Mitaa ya Barabara ya Kenyatta,

Machinjioni, Kawawa, Biafra, Starehe, Majengo, Zambia na baadhi ya sehemu za Ronsoti na Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya kikiwemo Chuo cha Ualimu cha Tarime. Utekelezaji wa Miradi hiyo umefanyika kuanzia mwaka 2007 hadi 2010 na kugharimu shilingi 1,001,202,879.

(b) Mheshimiwa Spika, mkakati wa kuongeza upatikanaji wa maji katika Wilaya ya Tarime ni pamoja na kujenga Miradi Mipy ya Maji ukiwemo uchimbaji wa visima kumi katika Vijiji kumi unaogharimu shilingi milioni 850 kuititia bajeti ya mwaka 2011/2012, kubadilisha miundombinu ya maji iliyochakaa, ujenzi wa chanzo cha maji kutoka Mto Mori na kuhimiza uvunaji wa maji ya mvua. Aidha, Mamlaka ya Mji wa Tarime imeweka mpango wa kupanua miundombinu ya maji kwa kutandaza mabomba katika maeneo yasiyo na maji. Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, zitatumika shilingi milioni 100 kutoka Wizara ya Maji kuititia Mamlaka ya Maji ya Mkoa wa Mara.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza ahadi za Viongozi kwa kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya Miradi ya Maji katika Wilaya ya Tarime. Bajeti ya Miradi ya Maji kwa mwaka imekuwa ikiongezeka kutoka shilingi milioni 22 mwaka 2007 hadi shilingi milioni 850 mwaka 2011/2012. Aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha kadiri zinavyopatikana kwa ajili ya Miradi ya Maji ili kutimiza azma ya kuwapatia Wananchi maji safi na salama.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ambayo kwa kiasi fulani yanaweza yakatia matumaini lakini sina uhakika kama yamefanyiwa utafiti wa kutosha hasa kwa asilimia 30 Wananchi wa Tarime wa Vijiji kupata maji safi na salama na asilimia 52 kupata maji safi na salama. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Wilaya ya Tarime imebahatika kuwa na vyanzo vya maji mfano Mto Mara ambao nina uhakika kabisa kwamba ukitumiwa vizuri utasambaza maji karibu katika Vijiji vyote vinavyozunguka Wilaya ya Tarime. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba inatumia maji ya Ziwa Victoria au ya Mto Mara kuwanufaisha Wananchi wa Tarime?

(ii) Mheshimiwa Rais, mwaka jana alipokuwa Tarime, aliwhakikishia Wananchi wa Tarime kwamba sasa tatizo la maji katika Mji wa Tarime na Vitongoji vyake litakoma katika kipindi cha mwaka huu. Serikali inasema nini kuhusu kauli hiyo?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Nyangwine, kwa namna anavyoshughulikia suala la maji katika Wilaya ya Tarime. Japokuwa swali lake alikuwa anasema kwamba, Wananchi hawajawahi kupata maji safi toka Uhuru; sasa kwa kumheshimu, ninaomba alirekebishe hilo kwamba Wananchi wamepata lakini si kwa kiwango kinachoridhisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kutatua tatizo la Tarime, Serikali hivi sasa imemwajiri mtaalam mshauri kwanza katika Mji wa Tarime pamoja na Mugumu, Mji Midogo, kuweza kufanya usanifu, tupate maji ya kutosha kwa miaka 20 ijayo. Wakati tunaendelea na hilo, tumekuwa tunapeleka fedha za kukarabati miundombinu iliyopo. Kwa hiyo, kazi hiyo bado inaendelea kama Naibu Waziri wa TAMISEMI alivyooleza.

Mheshimiwa Spika, sasa kuhusu kupata maji kutoka Ziwa Victoria, huyo Mtaalam Mshauri ndio kazi anayofanya. Ataangalia ni chanzo kipi tunaweza kupata maji ya kutosha kwa Vijiji vilivyo karibu na Ziwa Victoria na Mto Mara.

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu ya pili kuhusu ahadi za Rais; ninaomba nimhakikishie kwamba, kwa sababu Rais ameshaagiza na ameshaahidi, hilo ni agizo na sisi Watendaji tutafuata agizo la Rais, tutalitekeleza kama alivyoahidi.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwea Spika, ahsante sana kwa kuniona. Tatizo la maji katika Vijiji vingi hapa nchini linaendelea kuwa kubwa kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Ninaomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri; nimekuwa nikiuliza sana suala la matatizo ya maji katika

Wilaya ya Moshi hususan Kata ya Mbokomu, Vijiji vya Tera pamoja na Vijiji vya Kiwalaa mpaka leo tatizo ni kubwa sana, hakuna maji; ninaomba kujua mkakati wa Serikali katika kuhakikisha kwamba Vijiji hivyo vinapata maji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kama alivyosema kwamba, matatizo ya upatikanaji wa maji, hali ya hewa na matatizo ya tabianchi, yamechangia. Kwa hiyo, tuna kazi ya kufanya tuweze kuangalia kwamba tunatunza vyanzo vya maji ili tuweze kupata maji ya kutosha kwa ajili ya kuwapelekea Wananchi. Kwa hiyo, kazi hii ya kutunza maji ndiyo maana katika Sera ya Maji tumeweka Sheria Namba 11 ya 2009 kwamba, kila mmoja na hizi Jumuiya za Watumia Maji zifanye kazi ya ziada katika kutunza vyanzo vya maji ili maji haya yaweze kuwa endelevu kwa sababu hata chini ya ardhi sasa hivi upatikanaji wa maji unapungua siku hadi siku. Kwa hiyo, hii ni kazi ambayo ni endelevu, inabidi tuifanye sisi wote kwa pamoja.

Na. 100

Visima vya Maji Vinavyofanya Kazi Wilaya ya Mpwapwa

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE aliuliza:-

Katika kipindi cha 2005 - 2010 Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ilitekeleza Miradi mingi sana ya Maji ikiwemo ya Visima Vifupi, Visima Virefu na kukarabati Miradi ya zamani pamoja na Mradi Mkubwa wa Maji Mpwapwa Mjini:-

- (a) Je, ni visima vingapi vinafanya kazi hadi sasa?
- (b) Je, ni Miradi mingapi iliyokarabatiwa ambayo inafanya kazi hadi sasa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swalii la Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005 – 2010, Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilitekeleza Miradi Mipy ya Visima Virefu vinane, Visima Vifupi 86, Maji ya Mtiririko miradi mitatu na Uvunaji wa Maji ya Mvua miradi 15. Katii ya Miradi iliyojengwa, inayofanya kazi ni mitatu ya mtiririko, visima virefu minane, visima vifupi 77 na matenki ya uvunaji wa maji ya mvua 15.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya katika mwaka 2008 kwa kushirikiana na Wahisani wa Maendeleo, ilifanya ukarabati wa visima vitatu katika Vijiji vya Kibakwe, Mzase na Kisima kutokana na uchakavu wa miundombinu hiyo. Jumla ya shilingi milioni 141 zilitumika kwa kazi hiyo. Visima vyote vitatu havitoi huduma ya maji kutokana na kuharibika mara kwa mara kwa miundombinu ya maji yakiwemo mabomba na pampu zilizofungwa katika visima hivyo kutokana na kuwa na miaka mingi tangu vijengwe kwani vilijengwa miaka ya 1970 wakati wa uanzishaji wa Vijiji hivyo na kufuatia tetemeko la ardhi lilitokea katika maeneo hayo pia likasababisha tatizo hilo.

Wananchi wa Kibakwe kwa sasa wanapata maji kuititia vituo saba vilivyokarabatiwa kuititia uhisani wa WaterAid Katika chemchemi 20 zilizopo. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa katika bajeti ya mwaka 2011/2012 imeidhinishiwa shilingi 1,185,116,000 kwa ajili ya uchimbaji wa visima vipyta katika Vijiji vya Kimagai, Mzase, Kisima na Wiyenzele.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba tuliwahi kwenda naye na akazindua Mradi pale Kibakwe wa kisima kilichokarabatiwa. Nikuhakikishie tu kwamba mpaka leo

hii bado maji hayatoki pale, mlipoachana tu ulipoondoka, hali huku nyuma ikabadilika na mpaka leo jitihada zote pamoja na maneno yote lakini bado maji hayajatoka:-

(i) Ukizingatia mazingira hayo pamoja na tatizo la Lukole na Wiyenzele na sehemu zingine; mimi ninadhani masuala ya visima ni bora yakatiliwa mkazo kwamba ni vizuri utaratibu wa mashine zile mpya zinazonunuliwa ziwe na kigezo maalum cha aina ya mashine za kununua kwa sababu kilichotokea ni kwamba mashine zile zimekufa. Je, Mheshimiwa Waziri unasemaje?

(ii) Msingi mkubwa wa kuleta maji katika maeneo yetu ambayo tuna bahati ya vyanzo vya asili vya maji ya mtiririko, mimi ninadhani ni utunzaji wa mazingira. Mheshimiwa Waziri unatusaidiaje katika mkakati wa Kitaifa wa kutunza mazingira na unawaambia nini Wananchi wa Mpawala ili tuweze kufanya jitihada ya pamoja kulinda mazingira yetu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, mimi nimekuja na takwimu zote hapa na kila kitu. Kwanza, ninataka nikuthibitishie, anachosema Mheshimiwa George Simbachawene ni kweli na kama alivyosema, mimi nimekwenda; pale pana tatizo na tumeeleza hapa. Tulichokifanya pale, tumetengeneza ile pampu imekwenda upande, ukinyonya pale yanakuja maji na tope. Kwa hiyo, mimi siwezi kukaa hapa nikabishana na Mheshimiwa Simbachawene, ambaye ni Mwenyekiti wetu pia hapa nikasema hapana. Kwa hiyo, kuna matatizo. Anachozungumza hapa na tumesema chanzo cha maji sasa hivi wanachopatia maji ni kwenye chemchemi. Maji yale hayafai kwa sababu huwezi kujua kama yana kipindupindu au hayana.

Mheshimiwa Spika, anacho-address *Member of Parliament* hapa ni kweli ndiyo maana tumekuja hapa na hizo takwimu za bilioni 1.186 ambazo zimetengwa. Nimekwenda kwenye speech ya Mheshimiwa George Simbachawene, alioitoa wakati Wizara ya Maji inapitisha bajeti hapa, amelalamikia mambo haya haya. Anachozungumza mle ndani *in fact* amekata tamaa kabisa hata na Miradi ya *World Bank*. Mimi ninamwomba asikate tamaa, asiwe Tomaso, atuamini kwamba tume-register na mimi nimefika mpaka Kibakwe, nimeona matatizo yaliyoko pale. Tutashirikiana naye pamoja na mwenzetu wa Wizara ya Maji, kuhakikisha kwamba tatizo hili linaondoka.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo ameliulizia hapa juu ya vyanzo vya maji; mtu hahitaji kwenda Chuo Kikuu kujua kama watu wakienda kulima kwenye maeneo ambayo ni vyanzo vya maji, maana yake ni kwamba, hutapata maji. Mtahama wote, mtaondoka. Hili wala sina haja ya kumtafuta Dkt. Huvisa tuje tuzungumze hapa, watu ambao wamekwenda kujenga katika vyanzo vya maji, ukisoma zile sheria ndogo ndogo za Mpwapwa, mle ndani utakuta zimeandikwa ni marufuku mtu kwenda kujenga katika chanzo cha maji. Mkijenga katika chanzo cha maji, watu watahama, patakuwa jangwa. Kwa hiyo, ninachotoa hapa ni maelekezo; Mkurugenzi Mtendaji wa Mpwapwa, kwa niaba ya Waziri Mkuu, aende akaangalie eneo linalozungumziwa hapa. Akikuta watu wamekaa katika vyanzo vya maji, *there is no compromise*, ahakikishe kwamba wanaondoka. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Hamad Rashid, wengine hamkusimama kabla! (*Kicheko*)

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, tatizo la maji limekuwa kubwa kila mahali na wenzetu wengine ambao wamegundua kwamba kuna matatizo ya maji, wameangalia katika hewa kuna maji mengi sana ya kutosha. Kwa mfano, Waisraeli wamegundua maji hayo na wana mashine wanazalisha zinaweza kutoa lita 5,000 kwa saa 24. Je, kwa nini Serikali haiagizii teknolojia hii ili kupunguza tatizo la maji hasa katika shule na kadhalika?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli zipo teknolojia mbalimbali ambazo tunaweza tukazitumia ili tuweze kuongeza upatikanaji wa maji na kama hiyo aliyoisema. Kwa hiyo, Wizara yangu italiangalia hilo pamoja na teknolojia zingine za kuchukua maji ya chumvi ili tuweze kuongeza upatikanaji wa maji.

Kuboresha Kituo cha Polisi Wilaya ya Kimara

MHE. JOHN J. MNYIKA aliuliza:-

Kata za Kibamba, Kwembe, Mbezi, Msigani, Makuburi, Saranga na Kimara katika Jimbo la Ubungo zinatumia Kituo cha Polisi Wilaya ya Kimara ambacho kinakabiliwa na changamoto nyingi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha Kituo hicho kama vile kuongeza vyumba, vifaa na motisha kwa askari?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kituo chenye hadhi ya Daraja B au hadhi ya Wilaya katika Jimbo la Ubungo?

(c) Je, kwa nini Serikali isitoe ruzuku kwa ajili ya ulinzi shirikishi ili kuongeza nguvu katika michango inayotolewa na Wananchi kama sehemu ya utekelezaji wa mkakati wa Polisi Jamii?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Ubungo, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya, Jengo la Kituo cha Polisi Kimara lipo katika hifadhi ya barabara (*Road Reserve*). Kwa maana hiyo, hatuwezi kuongeza vyumba pale. Hata hivyo, tutaongeza vitendea kazi pamoja na kuboresha maslahi ya askari.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango wa kujenga Kituo cha Daraja A katika Wilaya ya Kipolisi Kimara. Kwa sasa, juhudzi za kupata eneo la ujenzi wa kituo hicho zinaendelea. Nimwombe Mheshimiwa Mnyika, atusaidie katika harakati hizi za kupata eneo.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali haijatenga fedha kwa ajili ya Ulinzi Shirikishi au Polisi Jamii kutokana na uhaba wa rasilimali fedha. Dhana yenye inawataka Wananchi na wadau wengine kushirikiana na Serikali kuimarisha ulinzi na usalama kwa kuzingatia kwamba, Jeshi la Polisi peke yake haliwezi kufanikiwa bila kuwashirikisha wadau wengine. Ninatambua michango mingi na mikubwa inayofanywa na Wananchi mbalimbali nchini katika kuimarisha dhana ya Ulinzi Shirikishi na Polisi Jamii katika Taifa letu.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwamba, Naibu Waziri ameleeza ukweli kwamba, Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kimara kilichoko pale Mbezi kwa Yusufu kipo kwenye eneo la barabara. Sasa swali la nyongeza la kwanza:-

(i) Je, Serikali sasa ipo tayari kwa kuwa sisi tupo tayari kutoa msukumo kuandika rasmi kwa Manispaa ya Kinondoni kuomba eneo ikitoa *specification* ya mahitaji ili tuweze kuhakikisha eneo linapatikana haraka kwa sababu nimekwenda kwenye hicho Kituo Novembra 5 wakati Viongozi walipokamatwa pamoja na nyaraka za Katiba; kwa kweli hali ni mbaya, Askari Polisi wanajisaidia mpaka kwenye nyumba za jirani?

(ii) Je, Serikali ipo tayari sasa kuiandikia Manispaa ili taratibu hizi ziweze kufanyika?

(iii) Katika swali langu la msingi nililiza kuhusu maslahi ya askari na katika majibu ya Waziri ameleeza kwamba, Serikali ipo tayari kuboresha maslahi ya Askari; ningependa kufahamu; katika hatua hizi za kuboresha maslahi ya askari; je, Serikali ipo tayari sasa kushughulikia madai ya askari ya muda mrefu mathalani hivi sasa askari waliahidiwa kulipwa posho ya *rationing allowance* ya shilingi laki moja na hamsini lakini wanalipwa shilingi laki moja. Askari walikuwa wakienda

kufanya gwaride wanalipwa kwa mwezi shilingi laki tatu lakini sasa tunapoelekea Maadhimisho ya Uhuru wanalipwa shilingi elfu themanini peke yake. Askari wa FFU wana madai ya muda mrefu sana, wengine waliostaafu mpaka sasa hawajalipwa madai yao wamenga'ng'anisa mpaka walipwe maslahi yao; ningependa kupata jibu kutoka kwa Waziri kwa sababu askari hao wamekuwa wakitumia njia za kawaida kudai lakini wamekuwa wakitishwa na wamekuwa wakitakiwa kuacha mambo haya; sasa ningependa kujua ili askari nao wasije kugeuka kama Walimu kwenda kushiriki kwenye migomo na maandamano?

Ningependa kupata jibu kutoka Serikalini.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali ya nyongeza mengi tu ya Mheshimiwa Mnyika, kama ifuatavyo:-

SPIKA: Unajibu maswali mawili tu, ndiyo Kanuni.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kuhusu swalii la kwanza, ninafikiri utaratibu huu upo mbioni wa kupata barua na ninadhani kuna barua ilikuwa imekwishaandikwa kama sikosei, lakini hilo tutalifuatilia kwa sababu eneo ni lazima lipatikane na katika hili ndiyo maana nikasema kwamba, ushirikishwaji wako wewe Mbunge utakuwa ni muhimu, kuhakikisha kwamba eneo linapatikana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la maslahi ya Askari wetu, umezungumza mambo mengi, lakini niseme tu kwamba, kuna mambo mengine Mheshimiwa Mbunge ungeyafanyia utafiti wa kina kabla hujaja kuyaweka hadharani hapa kwa sababu yanajenga chuki na yanaleta mtafaruku kati ya Serikalini na Askari wake ambalo si jambo jema.

Mathalani, tumekuwa tunasema maboresho yanafanyika kwa sababu posho ya askari imepandishwa na hii tuliyozungumza kwamba itoke kwenye shilingi laki moja mpaka shilingi laki moja na hamsini; ni jambo ambalo tunalo na tumelifanyia kazi na tuna uhakika kwamba, litaweza kutimia. Kubwa katika suala la maslahi tuisitazame askari peke yake, kuna askari, walimu, madaktari, manesi na kadhalika na hii yote inategemeana na hali halisi ya uchumi tulionao nchini. Tutajitahidi kadiri uchumi utakavyoruhusu, siyo hao tu hata mishahara ya Wafanyakazi wa Serikalini na pengine pote, hapana shaka itaboreshwya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la gwaride; hili ni suala ambalo limeletwa kwetu sisi, siyo suala ambalo linalihusu nchi nzima. Yamekuwepo malalamiko kutoka kwa baadhi ya askari kwamba ni Dar es Salaam peke yake, lakini kule mikoani bado ahadi ambazo walipewa juu ya posho zao zinakwenda sawasawa, lakini kuna hitilafu katika Mkoa wa Dar es Salaam na ni jambo ambalo tunalifanyia kazi. Kwa hiyo, tusichukulie kwamba ni jambo ambalo linalokea nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wastaafu; wastaafu wenyewe matatizo siyo wengi, tatizo ambalo limejitokeza ni kwamba, kumekuwa na tatizo la utunzaji wa kumbukumbu na hapo ndipo tunesema kwamba ninataka nikiri kwako nitakuwa siyo mkweli. Kumekuwa na udhaifu kidogo upande wa Polisi Makao Makuu, upande wa Utawala, katika kuhakikisha kwamba rekodi zinawekwa sawasawa. Marekebisho yamefanyika pale na kuna baadhi ya Wafanyakazi wameweza kubadilishwa kuhakikisha kwamba kero kama hii haitendeki tena. Tunajiuiliza kwa nini inatokea upande wa polisi peke yake lakini maeneo mengine hali ya wastaafu wanapokwenda kudai mafao yao inakuwa sawasawa!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunajitahidi na masuala yako ni muhimu na *interest* za askari wetu tunazi-*take into account* wakati wote.

SPIKA: Maswali mrefu na majibu mrefu tunaendelea na swalii linalofuata.

Ahadi ya Kupandishwa Vyeo kwa Maafisa Wawili wa Kikosi cha Zimamoto

MHE. WARIDE BAKARI JABU aliuliza:-

Tarehe 22 Januari, 2004 kulipotokea moto mkubwa katika Kituo cha Mafuta cha TANESCO Ubungo na kufanikiwa kuzimwa na Kikosi cha Zimamoto, aliyekuwa Waziri Mkuu wakati huo aliagiza kupandishwa vyeo Maofisa wawili walioshiriki kuzima moto huo, ambapo mmoja wa Maafisa hao tayari ameshapandishwa cheo tangu tarehe 24 Aprili, 2004:-

(a) Je, ni lini Serikali itampandisha cheo cha Afisa huyu mwingine ambaye bado hajapandishwa?

(b) Je, ni sababu gani zilizosababisha huyu Afisa mmoja kutopandishwa cheo hadi leo hii?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mbunge wa Kiembesamaki, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli aliyekuwa Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Awamu ya Tatu, aliagiza Maafisa wawili walioshiriki kufunga valve chini ya matanki ya Kituo cha TANESCO Ubungo na kuepusha madhara makubwa kutokea wapandishwe vyeo.

Mheshimiwa Spika, Afisa huyu mwingine aliyekuwa na Cheo cha Mrakibu wa Zimamoto na Uokoaji, alipandishwa cheo na kuwa Mrakibu Mwandamizi wa Zimamoto na Uokoaji tarehe 1 Julai, 2006. Aidha, katika kikao cha hivi karibuni cha Kamati Maalum ya Ajira ya Wizara, Afisa huyo amepandishwa cheo na kuwa Kamishna Msaidizi wa Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuwapandisha vyeo Maafisa wa Majeshi yetu chini ya Wizara ya mambo mbalimbali ikiwemo uwepo wa nafasi wazi iliyotengwa katika Ikama ya mwaka husika, kuiva kwa Afisa husika ili kuweza kupanda cheo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, pamoja na Watumishi hao kupandishwa vyeo, kwa kutambua mchango wao, tarehe 26 Aprili, 2007, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliwatunuku watumishi hao Nishani ya Ushupavu.

MHE. WARIDE BAKARI JABU: Mheshimiwa Spika ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ninapenda kumwuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa uamuzi wa kupandishwa cheo askari mmoja ulichukua miaka minane; je, Serikali haioni tendo hili litasababisha kuondoa upendo na jitihada katika kazi za uokoaji majanga?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ni kweli imechukua muda, lakini kuchukua muda ni kutohana na Idara ya Zimamoto imekuwa inahamahama, maana tangu ule mwaka ambao Waziri Mkuu alitamka vile mwaka 2004 mpaka wakati huu, imepitia katika sehemu mbalimbali mpaka kuja kuingia katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kikubwa, ninataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, hapa kwa kweli kidogo kulikuwa kuna ulegevu wa utekelezaji na katika hilo niseme kwamba, tunaomba radhi.

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Nimemsikiliza vizuri Naibu Waziri akijibu, sikusikia kama yule askari wa pili amepandishwa cheo, nilichokisikia ni kwamba mwaka juzi kapewa Nishani na Rais wakati agizo la Waziri Mkuu ilikuwa ni kupandishwa cheo.

Sasa labda tupate tu uhakika kwamba na yeye atapandishwa cheo au hizo taratibu za kawaida za kumpandisha cheo yeye sifa hazitosh?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ni kweli wakati ule hawa askari walikuwa wapo katika mamlaka ya Wizara kwa maana ya kusema kwamba, Kamishna wao wa Polisi alikuwa anaweza kuwapandisha vyeo, lakini kwa sababu muda umepita na nafasi yake imebadilika, basi ile nafasi anayeweza akapandisha cheo hicho ipo katika mamlaka ya Rais.

Mheshimiwa Spika, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kilichofanyika ni kwamba, jina lake limewekwa katika majina na hilo ndiyo jibu sahihi na nimhakikishie huyo askari atakuwa anasikia Waziri wa Wizara anajibu swali hilo; tuna uhakika kwamba Rais ataridhia na atawenza kupata cheo chake hicho. Kwa sababu kama nilivyosema, huo ni uamuzi wa Rais na siyo uamuzi wa Wizara tena.

Na. 103

Kurasimisha Mafunzo ya Udereva Daraja 'C' VETA

MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MHE. MOHAMED G. DEWJI) aliuliza:-

Ili kupata leseni ya udereva Daraja la 'C' ni lazima usome kwenye Chuo cha *NIT*; na waombaji wengine wa leseni za daraja hilo hawana uwezo wa kuhudhuria mafunzo hayo:-

Je, Serikali haiwezi kurasimisha mafunzo hayo kwenye Vyuo vya VETA nchini ili kuwawezesha wahitaji wengi zaidi kuhudhuria mafunzo hayo kwa urahisi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo wa Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Gulam Dewji, Mbunge wa Singida Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali imeshaviruhusu Vyuo vya VETA kutoa mafunzo hayo na yanaendelea kutolewa katika Mikoa mbalimbali nchini.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Pamoja na madereva kupata kozi kikamilifu lakini bado ajali zipo barabarani; je, Serikali ina mikakati gani ya makusudi kuhakikisha ajali hizi sasa zinapungua kuliko ilivyo sasa?

(ii) Kwa kuwa hata waenda kwa miguu, waendesha baiskeli na wasukuma matoroli wamekuwa ni chanzo mojawapo cha ajali barabarani na alama za waenda kwa miguu zipo mijini tu; je, Serikali haioni kwamba kuna kila sababu sasa kuweka alama za waenda kwa miguu na baiskeli kwenye barabara zote pamoja na kutoa elimu kwa Wananchi wote ili waweze kwenda kwenye alama walizowekewa na kupunguza ajali ambazo zinajitokeza mara kwa mara?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa kweli tunafanya jitihada na ndiyo maana tumebadilisha hata mfumo sasa wa kupata leseni, kwa sababu leseni nyingi zilikuwa zinaghushwa na nyingi walizokuwa wakipewa wanaponyang'anywa leseni, bado walikuwa wanawenza wakaenda mikoa mingine wakapata leseni. Kwa hiyo, tunajaribu kuweka utaratibu ambao tutakuwa na uhakika wa kuona nani anapata leseni na anapata kutokana na mafunzo na utaalam ambao ameujenga na hili suala ni kubwa na linatutesa vichwa yetu.

Niseme kwamba, hatuwezi tukaachia askari peke yake ama tukawaachia mamlaka peke yake; ni suala shirkishi kwa maana ya kusema kwamba, wale abiria kwa mfano wanapokuwa katika magari na hususan tunapozungumzia mabasi ambayo yanasafirisha abiria, nao wawe

wanashirikiana na uongozi na ndiyo maana kwenye mabasi yote sasa tumeweka namba za *Regional Traffic Officers (RTO)* wa mikoa yote, endapo wataonekana madereva wanakwenda mwendo kasi na kama itaonekana madereva wanakwenda kinyume, basi itabidi hatua zichukuliwe kwa kupiga simu na kuwataarifu *RTOs* katika maeneo mbalimbali hatua ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili linatazamwa katika Baraza la Usalama la Taifa kuona ni njia gani pia tunaweza tukazichukua, kwa sababu hili ni suala ambalo limekuwa gumu na linaleta matatizo kwa sababu vifo vya raia wetu vinakuwa vingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalii lake la pili, ninakubaliana naye kwamba, alama zisambazwe mbali na mijini, lakini hata huko vijiji ni ziwekwe. Niseme kwamba, hapa tutaomba ushirikiano wa Halmashauri, tutaomba ushirikiano wa Wabunge na Madiwani, kwa sababu hili ni letu sote, tukisema kwamba tunaliachia Serikali Kuu peke yake, ninadhani kidogo hapo itakuwa ni mzigo mkubwa, lakini tukiweza kushirikiana sote kwa pamoja, tunaweza tukakabiliana na hali hii ambayo siyo nzuri katika Taifa letu.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Spika ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii moja la nyongeza.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Swalii la pili sijajibowi la waenda kwa miguu.

SPIKA: Ngoja kwanza, Mheshimiwa Maida uliza kwanza.

MHE. MAIDA HAMADI ABDALLAH: Kwa kuwa wapo madereva wazoefu ambaa hapo awali walipatiwa leseni Daraja la C; na kwa kuwa kwa sasa walitakiwa kurudisha leseni hizo na badala yake wapatiwe Daraja D; je, Serikali haioni kwamba upo umuhimu wa kuandaa utaratibu mwingine kwa madereva ambaao ni wazoefu na hapo awali walipatiwa Daraja C wanaporejeshewa leseni hizo wakaendelea kururejeshewa Daraja C ili kuondoa usumbufu kwa wale ambaao kwa sasa wameshakuwa watu wazima hawawezu tena kumudu gharama za masomo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, na hilo la watembea kwa miguu utaendelea hapo hapo. Ninaomba ujibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, hili swalii la watembea miguu nimelijibu; limeulizwa kwamba alama ziwekwe kule vijiji kwa sababu zipo mijini tu kwa waenda kwa miguu na waendesha balskeli na kadhalika. Nikasema kwamba, inataka ushirikishwaji wa wengine wote na siyo mamlaka peke yake kuhakikisha kwamba hili linatendeka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la leseni, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge jamani chonde chonde, hapa tunachokizungumzia ni uhai wa Watanzania na kumekuwa na mambo mawili yanajitokeza ndani ya Bunge hili. Jambo la kwanza ni lile la kusema kwamba, watu wahurumiwe wasipitie katika mambo ya mitihani kwa sababu ya suala la ajira.

Hii ni ajira ambayo ni tofauti; hawa wanakwenda na roho za Watanzania mikononi mwao. Kwa hiyo, ninataka kusema kwamba, katika hili hakuna *compromise*, utaratibu uliowekwa utafuatwa, mitihani itafanywa, wale ambaao wataonekana kweli wanastahili kupata leseni watapata, wale watakaoonekana hawastahili kupata leseni hawatapata.

Na. 104

Ujenzi wa Barabara ya Tanga – Pangani – Makurunge

MHE. SALEH A. PAMBA aliuliza:-

Katika llani ya Uchaguzi ya Mwaka 2010 - 2015 Barabara ya Tanga – Pangani – Makurunge, yenye urefu wa kilomita 178 imepangwa kujengwa kwa kiwango cha lami:-

Je, ni lini ujenzi wa Barabara hiyo utaanza?

SPIKA: Ahsante. Waziri majibu. Leo Waziri huyu ni Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni pia. (*Makof*)

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Saleh Ahmed Pamba, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo:-

SPIKA: Tunahitaji utulivu humu ndani ya Bunge.

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE): Mheshimiwa Spika, Barabara ya Tanga – Pangani – Makurunge (Bagamoyo) ni sehemu ya barabara inayoendelea kufanyiwa upembizi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami chini ya Mradi wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC), unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), ambao unahuishisha barabara za kutoka Malindi – Mombasa hadi Lunga Lunga kwa upande wa Kenya na Tanga – Pangani – Makurunge Bagamoyo kwa upande wa Tanzania. Kazi za usanifu zimepangwa kukamilika mwezi Mei, 2012.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kazi ya usanifu kukamilika, Serikali za Tanzania na Kenya kwa pamoja zitatafuta fedha za ujenzi wa Miradi hii.

MHE. SALEH A. PAMBA: Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Waziri kwa majibu mazuri na yenye matumaini. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Barabara hii ya Tanga – Pangani – Makurunge ni kiungo muhimu cha usafiri kwa Wananchi wa Pangani na Mikoa mingine; na kwa kuwa Barabara hii wakati wa masika huwa haipitiki kabisa:-

(a) Je, Waziri anawaambia nini Wananchi wa Pangani kuhusu Barabara hii?

(b) Kwa kuwa Barabara hii inajengwa kwa ufadhili wa EAC na ADB na Wafadhili mbalimbali ambao watajitokeza; na kwa kuwa kuna viashiria kwamba hali ya uchumi duniani itakuwa na mtikisiko na hivyo kupunguza uwezo wa Wafadhili katika kutoa misaada yao. Je, Waziri atakubali kuiweka barabara hii katika kipaumbele ili ijengwe kwa fedha zetu za ndani iwapo fedha za Wafadhili hazitapatikana?

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE): Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Barabara ya kutoka Pangani hadi Bagamoyo, yenye jumla ya kilomita 178 ni muhimu sana kwa maendeleo ya Wananchi wa maeneo hayo hasa Pangani, lakini pia ina umuhimu wa pekee katika barabara zilizo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; na ndiyo maana sababu kubwa imeamuliwa ianze kufanyiwa *feasibility study* na *detail design* kwa pamoja kwa kushirikiana na wenzetu wa Kenya, ambapo jumla ya dola milioni 2.294 zinatumika kwa ajili ya kazi hiyo. Kampuni inayofanya kazi hiyo inaitwa *Airon Ameir Ltd.* kutoka South Africa.

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na yeze kwamba, kuna mtikisiko wa hali ya uchumi, lakini mtikisiko wa uchumi kama utawatikisa Wafadhili, utawatikisa pia Watanzania. Kwa hiyo, sisi tutaendelea kutafuta fedha kwa kushirikiana na Wafadhili mbalimbali na nina uhakika Wafadhili hawawezi kukataa na hasa baada ya *ku-meet zile qualification* baada ya *design*. Niapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Pamba, kwa kufuatilia kwa karibu sana barabara zinazohusu Wilaya yake ya Pangani.

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Spika ahsante. Katika Bunge lako Tukufu Waziri wa ujenzi aliahidi kwamba itakapofika mwezi Novemba, 2011kipande cha kilomita sitini kutoka Nyamwage mpaka Somanga kitakuwa kimekamilika na sasa mvua za masika zimeanza na athari hii ya mvua ilianza kuonekana katika kipindi cha mwaka uliopita:-

Je, Waziri analiambia nini Bunge hili juu ya tatizo ambalo linakwamisha kumalizika kwa kipande kile takriban sasa ni miaka mitatu?

SPIKA: Mimi nilijua tu utauliza hiyo hiyo.

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE): Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Barwany, Mbunge wa Lindi, kama ifuatavyo:-

Pamoja na kwamba, swali la msingi lilihusu Barabara ya Pangani hadi Bagamoyo, yenyе jumla ya kilomita 178, swali aliloliuliza Mheshimiwa Mbunge ni la kuhusu Ndundu – Somanga, yenyе jumla ya kilomita 56. Ninapenda kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, sehemu ile ya Somanga – Ndundu, ambayo inajengwa na Kampuni ya Kharafi, kwa ghamrama ya shilingi bilioni 60 na mkandarasi anaendelea na kazi, itakamilika kulingana na masharti ya Mkataba. Palikuwa na matatizo kidogo ya fedha, lakini kama wiki mbili zilizopita tulimlipa shilingi bilioni tatu.

Tunapanga wiki ijayo tutamlipa tena fedha zingine kutokana na madai yake. Tatizo la Mradi ule ni kwamba, mwanzoni ulikuwa unafadhiliwa na Benki ya Kuwait, baadaye fedha hazikutolewa na Benki ya Kuwait ikabidi fedha zote za Mkataba zitolewe na Serikali ya Tanzania.

Ninataka kuwashakishia Wananchi wa Kusini kwamba, barabara hii itakamilika kulingana na masharti ya Mkataba na ninamwagiza mkandarasi afanye kazi kwa juhud zote, kwa sababu anaendelea kulipwa fedha. (*Makof*)

SPIKA: Na mimi nimeshuhudia.

Na. 105

Ujenzi wa Barabara ya Mpemba Hadi Isongole Darajani

MHE. ALIKO N. KIBONA aliuliza:-

Katika ziara yake ya kikazi Wilaya ya Ileje Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiwa katika Daraja la Kimataifa liliopo kati ya Tanzania na Malawi na Mji wa Isongole aliahidi kuwa Barabara ya Mpemba hadi Isongole Darajani itajengwa kwa kiwango cha lami:-

Je, ni lini ujenzi wa Barabara hiyo utaanza rasmi?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, Mbunge wa Ileje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maandalizi kwa ajili ya kujenga Barabara ya Mpemba – Isongole yenyе urefu wa km 51.5 yamekwishaanza. Katika Mwaka wa Fedha wa 2009/2010, Barabara hiyo ilifanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa awali (*Feasibility Study and Preliminary Design*). Aidha, katika bajeti ya mwaka 2011/2012, kiasi cha shilingi milioni 93.55 kimetengwa ili kuendelea na kukamilisha usanifu wa Barabara hii na mchakato wa kumpata Mhandisi Mshauri (*Consultant*) wa kufanya kazi hiyo, umeanza kupitia Wakala wa Barabara Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya usanifu wa kina (*Detailed Engineering Design*) kukamilika, Serikali itaanza kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninayo maswali madogo mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nionavyo kiasi cha shilingi milioni 93 ni kidogo kwa kazi ya usanifu, lakini hata hivyo kwa sababu amesema ni kwa ajili ya kukamilisha, ninaamini wataalam walikuwa makini katika hilo. Je, kazi hii ya usanifu itakamilika lini na ni nani anayeifanya?

(b) Mheshimiwa Spika, Barabara ya kutoka Mpemba mpaka Kasumulu Boarder kule Kyela inapita mpakani mwa Malawi na Tanzania na ni barabara ya Kihistoria; umuhimu wake ni mkubwa kwa uchumi kwa hivi sasa. Mwanzoni ilijengwa kama ya ulinzi lakini sasa ni ya uchumi. Ninaomba kuuliza kwa kuwa Wananchi wa Kyela wanategemea bidhaa mbalimbali kutoka lleje na vivyo hivyo Wananchi wa lleje wanaitegemea Barabara hiyo; na kwa kuwa Barabara hiyo inapita kwenye miteremko mikali na inahitaji kuweka utengenezwaji ambao utakuwa wa kudumu; je, inaweza kuingizwa kwenye Mpango wa Serikali kuwekewa lami hapo baadaye?

SPIKA: Swali ilikuwa ni lami tu mengine yote yalikuwa ya nini?

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE): Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kibona, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa kwa ajili ya kufanya *feasibility study* kwa Barabara aliyoitaja ya Mpemba hadi Isongole zinatosha. Mhandisi Mshauri anayefanya kazi hiyo ni *Inter Consult Ltd.* ya Dar es Salaam kwa gharama ya shilingi milioni 232.184 na fedha hizi zote zilizotolewa ni fedha za ndani.

Katika fedha hizo, tumeponga pia fedha zingine ambazo zitatumika kwa ajili ya kufanya matengenezo ya kawaida katika kuhakikisha kwamba, hii barabara inapitika. Katika bajeti ya mwaka huu kuna shilingi milioni 182.5.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutengeneza tena barabara nyingine ya lami ya kutoka Isongole kuititia Ngana hadi Kasumulo ambayo ameiomba Mheshimiwa Mbunge; ni vigumu kwa barabara zote za Tanzania kutengenezwa kwa kiwango cha lami. Kwa mfano, Barabara ya Mpemba hadi Isongole imepandishwa daraja mwaka 2009 na kuwa Barabara Kuu; lakini kuna Barabara Kuu nyingi nchini ambazo bado hazijajengwa kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, tusubiri kwanza tumalize Barabara Kuu za kutoka Tunduma - Sumbawanga, Mpanda - Kigoma zitengenezwe kwa kiwango cha lami, Barabara ya kutoka Babati - Dodoma - Iringa imalizike kwa kiwango cha lami na Barabara zingine Kuu, halafu zingine za kwenda Isongole na Kasumulu zitafuata baadaye. Ninaomba Wananchi waelewe hivyo, kwa sababu uwezo wa Serikali hauwezi ukatengeneza barabara zote kwa kiwango cha lami.

Na. 106

Kupeleka Umeme Makao Makuu ya Wilaya Mpya

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE aliuliza:-

Serikali imeridhia kuanzhwa kwa Wilaya mpya katika Mkoa wa Kigoma zikiwemo Wilaya za Kakonko, Uvinza na Buhigwe:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Miji hiyo na Vijiji vinavyoizunguka?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya za Kakonko, Uvinza na Buhigwe ni kati ya Wilaya mpya 19 zilizotangazwa mwaka jana na Serikali na zinasubiriwa kuanza kazi rasmi ikiwa ni pamoja na uteuzi wa Viongozi na Watendaji wa Taasisi zake mbalimbali. Aidha, maamuzi yanashubiriwa kuhusu wapi pawe Makao Makuu ya kila Wilaya. Kama niliyoyeleza wakati nikijibu swali la Mheshimiwa David

Kafulila, utaratibu wa Serikali ni kuhakikisha kwamba, Makao Makuu ya Wilaya zote yanapatiwa umeme kwanza. Baada ya hapo, usambazaji wa huduma hii unaelekezwa kwenye maeneo mengine ndani ya Wilaya hizo. Hivyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, chini ya utaratibu huo, Wilaya hizi zitafikishiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna kazi inaendelea katika Mkoa wa Kigoma ya kufikisha umeme katika Miji ya Wilaya ya siku nyingi ambazo ni Kasulu na Kibondo. Katika Wilaya hizo, ujenzi wa mifumo ya usambazaji umeme unaendelea katika Makao Makuu ya Wilaya hizo mbili na unatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2012. Ujenzi wa Vituo vya Kufua Umeme Kasulu na Kibondo ulikwishakamilika tangu mwezi Januari, 2011.

Mheshimiwa Spika, baada ya shughuli hizo za usambazaji kukamilika, jitihada zitahamia katika Makao Makuu na Miji ya Wilaya Mpya za Kakonko, Uvinza na Buhigwe na kusambazwa katika vijiji vinavyoizunguka miji hiyo na vile vijiji vikubwa na vidogo vinaweza kuunganishwa kwa gharama ndogo na haraka na pia kutegemea na vigezo vingine vinavyotolewa wakati wa kufanya maamuzi, vigezo vya kiufundi, kiuchumi na kijamii.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Kwanza kabisa, kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya ya Kasulu na Wilaya ya Kibondo, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi, chini ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi na kufunga umeme wa jenereta katika Wilaya mbili za Wilaya Kasulu na Kibondo. Baada ya shukurani zangu ni swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa kitendo cha kukamilisha Mradi wa Umeme katika Wilaya ya Kibondo na Kasulu kimeleta hamasa kubwa kwa Wananchi kutaka kuunganishiwa umeme tofauti na maombi ya awali; je, Serikali inawaahidi nini Wananchi wa Wilaya ya Kasulu na Wilaya ya Kibondo pamoja na Vitongoji vyake vikiwemo Vitongoji vya Mwilanywa na Murusi ambao wameomba lakini hawajaunganishiwa umeme? (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, ninapenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Josephine Genzabuke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba uniruhusu nimshukuru kwa pongezi alizozitoa, kwa jitihada kubwa iliyofanyika kwa kupeleka umeme. Alikuwepo miaka mitano iliyopita na anajua kazi iliyofanywa na ukubwa wake. Kwa hiyo, ninaomba nipokee pongezi hizo kwa niaba ya Wizara na TANESCO. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hili la Kibondo na Kasulu ni kweli kwa sasa umeme uliokuwepo kwa jenereta za Kibondo na umeme ulikuwepo kwa jenereta za Kasulu ni mwingi sana, kulingana na matumizi ya pale. Tatizo tulilolibaini ni kwamba, kwa sababu ahadi ilichelewa kidogo, watu wengi walishindwa kujandaa kufanya taratibu za kuunganisha umeme.

Kwa hiyo, kilichotokea ni kwamba, sasa hivi baada ya kuona umeme umekuja pale Kibondo na Kasulu, maombi yamekuwa mengi sana.

Vilevile sasa pana jitihada za makusudi za kuunganisha kwa yale maeneo ya karibu. Kwa hiyo, hili jambo nimelipokea lakini ninamfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, kwa taarifa tuliyopokea hivi sasa ni kwamba, REA wanajandaa kutengeneza *bill of quantities* na kufanya tathmini ya jumla ya kujua kazi hizo mbili zitakwenda wapi pamoja na kupeleka umeme kuna eneo la Kabanga ambalo lilzungumzwa hivi karibuni nalo linafanyiwa kazi.

MHE. KAIKA S. TELE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa swali la msingi la Mheshimiwa Genzabuke linafanana sana na tatizo la umeme katika Mji wa Loliondo na Waso hasa kuhusiana na ukosefu wa nguzo za kusambazia umeme. Je, Serikali inafahamu tatizo hilo na inawaambia nini Wananchi wa Loliondo na Waso?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, ninaomba njibu swali la Mheshimiwa Telele, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tatizo hilo tunalifahamu na ninaomba nimhakikishie kwamba, nitamtafuta baadaye tuongee na Wataalam wa *TANESCO* na wahusika wote tuliokuwa tumewapa kazi ya kubaini ufumbuzi wa tatizo hili na Mheshimiwa Mbunge nitampatia majibu yanayostahili.

Na. 107

Kupeleka Umeme Makao Makuu ya Kata

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kupeleka umeme Kata za Ndala, Bukene, Itilo, Utwigu Nkiniziwa, Puge, Mizibaziba, Tongi na Ijanja?

(b) Je, katika utekelezaji wa ahadi hiyo Serikali itafikisha umeme kwenye Shule za Kata hizo, zahanati na vituo vya afya?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrew Kigwangwalla, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANESCO*, chini ya ufadhili wa Wakala wa Nishati Vijiji (*REA*), imekamilisha taratibu za uteuzi wa makandarasi wa ujenzi na usambazaji wa umeme kwenye Kata za Ndala na Bukene. Mkandarasi aliyeetuila ni *M/S NAMIS Corporate Ltd.* wa Dar es Salaam. Mkandarasi ameanza kuwasilisha baadhi ya vifaa vya Mradi na kazi ilianza mwezi Julai, 2011. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2012.

Mradi wa kupeleka umeme katika Kijiji cha Ndala utahusisha ujenzi wa kilomita 71.4 za njia ya umeme msongo wa Kv 33, urefu wa kilomita 28.655 za umeme mdogo wa KV 0.4 na ufungaji wa *transfoma* 14. Vijiji vilivyoko njiani kati ya Tazengwa Nzega hadi Ndala vitafaidika na Mradi huu. Vijiji hivyo ni Itiro, Utwigu, Mwanhala na Ngukumo. Vingine ni Nkiniziwa, Busondo, Utunguru, Puge na Kampala. Inatarajiwa Mradi utaunganisha umeme kwa wateja wapatao 420.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kupeleka Umeme Bukene utahusisha ujenzi wa kilomita 42.1 za njia ya umeme wa msongo wa KV 33, kwenye urefu wa kilomita 13 hivi za umeme mdogo wa KV 0.4 na ufungaji wa *transfoma* 11. Vijiji vilivyopo kati ya Nzega na Bukene vitakavyofaidika na Mradi huu ni Ijanja, Itobo, Busasi, Njiapanda na Itanana.

Inatarajiwa mpaka sasa hivi tathmini tuliyokuwa nayo ni kwamba, Mradi utaunganisha wateja wapatao 236. Uwekaji wa *transfoma* na utandazaji wa nyaya za njia ndogo unatarajia kuanza mwezi Desemba, 2011 na Mradi wote kukamilika Juni, 2012.

(b) Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Mradi huo, katika njia ya kwenda Ndala, vituo vya huduma za jamii vitakavyopata huduma ya umeme ni Zahanati za Busondo na Nkiniziwa na Kituo cha Polisi cha Puge. Hospitali ya Ndala vilevile ni moja ya walengwa wakubwa wa Mradi huu. Katika njia inayokwenda Bukene, Shule za Sekondari za Itobo na Bukene, zitapatiwa huduma ya umeme. Vilevile Kituo cha Polisi na Kituo cha Kusukuma maji vyote vilivyopo Bukene, vitapata huduma ya umeme.

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia nitambue kwamba, Serikali imetoa ahadi humu Bungeni ya muda mrefu ya kupeleka umeme Ndala na Puge. Hivyo, ninaomba niwapongeze Wananchi wa maeneo haya na niwahakikishie kwamba, pamoja na kufanya kazi ongezeko la upatikanaji

wa umeme nchini, jitihada za makusudi zitaelekezwa kwenye kuboresha usambazaji na hivyo maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge yatanufaika na utekelezaji wa mkakati huu.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, ninaishukuru Serikali kwa kutekeleza ahadi hii adhimu ya Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Pia ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Mradi huu unapita katika Vijiji vya Ijanija, Makomelo, Ngukumo, Mwambaha, Utwigu na Isalalo ambako kote kuna shule za msingi, shule za sekondari na zahanati na pia kuna Chuo cha Kilimo pale Mwanahala; kwa nini Serikali imechagua baadhi ya vijiji na kuvipelekea umeme kwenye sehemu muhimu za huduma kwa Wananchi na kuviacha vingine?

(b) Mwanzioni tulipata taarifa kwamba transfoma zilizoletwa Nzega zilifika 47 leo nimejumlisha katika majibu ya Mheshimiwa Waziri nimeona zimepungua na kubaki 25 tu; kwa nini upungufu huu umejitokeza?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Khamis Kigwangalla, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *line* ya umeme inapopita pale tumesema awali kwamba ni KV 33 halafu umeme ule unapozwa kwenye transfoma ndiyo tunaanza kusambaza kwenye KV 0.4 ambao ndiyo umeme unaoingia majumbani na kwenye maeneo kama haya. Kwa hiyo, kusema kweli lazima tuwe wakweli, hata huu Mradi ni mkubwa sana lakini mpaka hivi sasa tathmini iliyofanywa kwa vijiji vyote hivi ni wateja hawafiki 700.

Kwa hiyo, kuna vijiji hapa karibu 15 lakini wateja wenyewe ni 700 tu. Kwa hiyo, kinachoamua wapi pashuke umeme na wapi pasishuke umeme kama nilivyosema wakati ninajibu swalii la awali, kuna tathmini ya vigezo vya jamii, vya kiufundi na kadhalika.

Ninaomba nimuhidi Mheshimiwa Kigwangalla kwamba, lengo la *TANESCO* ni kupeleka umeme kwa Wananchi wengi kadiri itakavyokuwa. Sasa kama maombi yataongezeka katika suala hili na vijiji hivi, ninampa ahadi kwamba, *TANESCO* watalifanyia kazi na kama kutakuwa na wateja wengi zaidi watakaoomba kuunganishiwa umeme, watapata huduma hiyo ya umeme.

Mheshimiwa Spika, transfoma hizi kama zilikwenda 47na sasa zipo 25; hili suala kidogo lina *element* ya ufundi; kwa hiyo, inabidi ni-*consult* na *TANESCO* niwaulize. Inawezekana kwamba, transfoma zilizokwenda ziliikuwa kubwa au ndogo wakazibadilisha na transfoma kubwa, kwa hiyo, hili ni jambo ambalo inabidi wenyewe tuwaulize tujue ni mazingira gani ambayo yalipelekea wakapeleka transfoma 47 wakaona zinatosha wakati huo na sasa wakaona zinatosha transfoma 25. (*Makofi*)

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi hii. Ninaomba nimwulize Mheshimiwa Waziri; kwa sababu kumekuwa na ahadi ya muda mrefu kupitia Mpango wa *REA* ya kupeleka umeme katika Miji ya Fulo, Sumve, ambao sasa upo tayari lakini kipo Kijiji cha Ibindo, Marigis, Kabila na Nyashana; kupitia Mpango wa *REA* unaweza ukawaambia Wananchi wa Jimbo la Sumve kwamba umeme utapatikana lini? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, hilo swalii ni jipya kabisa na vijiji vipyta kabisa; kwa heshima wamesikia hao, kama unavijua jibu lakini ninaamini ni jipya mno.

Fidia kwa Wananchi Kupisha Upanuzi wa Uwanja wa Ndege - Majengo

MHE. SABREENA H. SUNGURA aliuliza:-

Ni mwaka mzima sasa tangu wananchi wa Kata ya Majengo (Manispaa ya Kigoma Ujiji) wafanyiwe tathmini ya makaburi yao ili kupisha eneo la upanuzi wa uwanja wa ndege:-

Je, ni lini wananchi hao watalipwa fedha zao ili upanuzi uweze kuendelea?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoo wa Kigoma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ilifanya tathmini ya makazi, mazao na makaburi yaliyopo katika Kata ya Majengo Wilaya ya Kigoma Mjini amesema Manispaa ya Kigoma Ujiji ili kujua kiasi cha fedha kinachotakiwa kulipwa ili kupisha upanuzi wa kiwanja. Tathmini hiyo iliyofanyika kwa mara ya kwanza mwaka 2007 na kuboreshwa tena mwaka 2009 ambapo ilionesha kuwa jumla ya shilingi milioni 870 zinahitajika kwa ajili ya zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali, zoezi la ulipaji wa fidia kwa wananchi wa Kata ya Majengo halitaweza kufanyika kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Badala yake zoezi hilo limepangwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2012/2013. Hivyo basi, tunaomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kata ya Majengo wawe wavumilivu na subira hadi wakati huo.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kutokana na majibu ya Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa suala hili ni suala la muda mrefu takribani miaka mitatu imekuwaje Serikali ipate fedha za upanuzi na ikose fedha za fidia?

(b) Waziri anawahakikishaje wananchi hawa kwamba Bajeti ya mwaka 2012/2013 itazingatia suala hili?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *ili-sign* Mkataba wa kufanya upanuzi wa kiwanja cha ndege Kigoma pale Majengo pia uwanja wa Tabora na Bukoba mwezi Septemba 2011, hivi sasa Mkandarasi wa kufanya upanuzi wa viwanja hivyo kikiwemo cha Kigoma ambaye ni *Sinohydro* ya China amekwisha kabidhiwa kazi hiyo na anendelea na *mobilization* itakayotarajiwa kuchukua miezi mitatu. Miradi hii inatekelezwa chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. Hivyo ni kweli kuwa Kiwanja cha Ndege cha Majengo kitapanuliwa.

(b) Mheshimiwa Spika, swalii la (b) ni kweli kuwa Serikali imepata fedha za ujenzi kabla ya fedha za kuwafidia wananchi. Kama nilivyosema sehemu ya (a) Serikali inajenga viwanja hivi vitatu kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia ambavyo utaratibu wake hautengi fedha za fidia, Serikali imepanga kuwalipa fidia wananchi katika kipindi cha mwaka 2012/2013, nimoimbe Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kigoma wawe wavumilivu kuruhusu ujenzi wa uwanja huu na upanuzi wa kiwanja hiki kwa manufaa makubwa ya Mkoo na Mji wa Kigoma kwa sababu shughuli zitaongeza ajira.

SPIKA: Ahsante, maswali yamekwisha, muda umekwisha. Mheshimiwa Naibu Waziri zile eeh! Zimekuwa sawasawa na swali lenyewe, zimekuwa nyingi sawasawa na jibu lenyewe kwa hiyo nadhani ujitalidi kupunguza hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza nataka kuwatambua, Wabunge naomba tusikilizane. Napenda kuwatambua wageni ambao tunao katika Ukumbi wetu; kwanza nianze na mgeni alieko kwenye *Speaker's Gallery* ni Mheshimiwa Pius Msekwa, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa. Kwa namna ya pekee Spika Mstaafu ndiye aliyeanzisha mradi wa jengo hili. Karibu sana Mzee, tunakushukuru. (*Makofii*)

Lakini tuna wageni wengine, katika Bunge letu leo tunao wanafunzi 72 kutoka Chuo cha Biashara *Campus* ya Mwanza na Dar es Salaam, naomba wasimame pale walipo wote, wanafunzi wa *Campus* ya Mwanza, hawapo? Basi wamekosa nafasi basi baadae. (*Makofii*)

Kuna wanafunzi 60 kutoka Chuo Kikuu cha *St. John* Dodoma, naomba msimame milipo hapo, ahsante sana mkazane kusoma, Chuo chenu kina sifa nzuri muendelee vizuri. Tuna wanafunzi 37 kutoka Chuo Kikuu cha *UDOM* na hawa wako wapi? Naomba wasimame walipo, aha! Ahsante sana mna *premises* nzuri sana hakikisheni mnazitunza na mnasoma kwa bidii. (*Makofii*)

Kuna wanafunzi 20 kutoka Chuo cha Mipango Dodoma na wenyewe wako wapi? Leo Dodoma yote ipo hapa, hawa wamekosa nafasi basi baadae. Kuna waandaaji 50 wa vipindi vyta elimu kwa umma kutoka taasisi mbalimbali za Serikali vinavyorushwa na *TBC Taifa* wako wapi hawa waandaaji wa vipindi? Aha! *Okay*, ahsante sana ndiyo maana vipindi vyetu tunavielewa vizuri, ahsante sana. (*Makofii*)

Tuna viongozi nane wa wanafunzi kutoka matawi yote matatu ya Chuo cha Biashara Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza, viongozi nane wa wanafunzi, hawa na wenyewe wako wapi? Nadhani wako pamoja na kundi lile, lakini hapa nina Mchungaji, haya ndiyo matatizo ya kuandika vikaratasi bila kuleta *formal*, nina Mchungaji John Kibuga na Msaidizi wake ndugu Samuel Daninga, naomba Mchungaji huyu asimame alipo, hawa wanatoka Iramba Magharibi, karibu sana Mchungaji na Msaidizi wako. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya kazi, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Edward Lowassa anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba watakuwa na kikao leo saa saba mchana katika Ukumbi namba 133 saa saba mchana. (*Makofii*)

Nina tangazo la Mwenyekiti Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa January Makamba anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo kutakuwa na kikao chumba namba 219 saa saba mchana. Pia Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Daudi Lembeli anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo pia watakuwa na kikao saa saba mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa B, halafu Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margaret Sitta anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana watakuwa na kikao katika Ukumbi wa *basement*, halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter Serukamba anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana watakuwa na kikao katika chumba namba 231. (*Makofii*)

Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dokta Augustine Lyatonga Mrema anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana watakuwa na kikao katika Ukumbi wa Msekwa C. (*Makofii*)

Halafu Mheshimiwa Jenista Mhagama, Katibu wa Kamati ya Wabunge wa CCM anaomba niwatangazie Wabunge wote wa CCM kuwa leo saa moja usiku watakuwa na kikao cha Kamati ya Chama, Ukumbi wa Pius Msekwa, hawa ni saa moja usiku, hii inatokana na kwamba tutahairisha kikao chetu saa saba mchana mpaka siku inayofuata kwa hiyo wenyewe saa moja usiku Kamati ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Halafu Kaimu Katibu wa TAPAC. TAPAC ni Chama cha Kupambana na UKIMWI cha Wabunge, huyu ni Dokta Faustine Ndugulile anaomba nitangaze kwamba Kamati ya Utendaji ya Chama cha Wabunge katika mapambano dhidi ya TAPAC inapenda kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa leo saa saba mchana, baada ya kuhairisha Bunge kutakuwa na kikao kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa, wanachama wote wa zamani na wapya wanaombwa kuhudhuria. Sasa hawa wanachama wote wa TAPAC saa saba mchana mtakuwa na kikao pale. (Makof)

Waheshimiwa Wabunge, nimemaliza matangazo ya kazi tunaendelea, Katibu.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011 (*The Constitutional Review Act, 2011*)

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wafuatao nadhani hata jana walitajwa, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Paul Lwanji, Mheshimiwa Livingstone Lusinde na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis ndiyo wataanza kuzungumza. Mheshimiwa Abdulkarim Shah.

MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nakushukuru kwa kunipa fursa hii kwa kuweza na mimi kuchangia Muswada huu wa Uundwaji wa Tume itakayosaidia uratibu mzima wa uundwaji wa Katiba yetu mpya. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nimponeze kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa kukubali uanzishwaji mzima wa mchakato wa uundwaji huu wa Katiba, naomba nimshukuru na kumpongeza kwa moyo wa ujasiri kwa sababu bila ujasiri angeweza hata kuiminyia akasema isubiri kwa sababu hii Katiba mpya inaweza ikanipunguzia madaraka, lakini alikaa, akafikiri na umri uliopita toka tupate Uhuru miaka 50 ni umri wa mtu mzima kama mimi hapa ina maana toka nilivyozaliwa mpaka leo siku ya kusimama kesho kutwa na mimi natimiza miaka 50 sasa ukubwa wa Katiba tuliyokuwa nayo ni sawasawa na umri wangu, mabadiliko yanahitajika katika baadhi ya vipengele sio mabadiliko ya Mbunge, *Inshallah* Mwenyezi Mungu atazidi kumpa imani, namuombea dua. (Makof)

Mheshimiwa Spika, wachangiaji waliokuwa wamechangia katika mjadala huu toka uanze ni 50 mpaka jana ni zaidi ya 45 mpaka 50 mpaka jana jioni. Katika vipengele vizima vifungu vilivyokuwa katika Muswada huu ni 34 kwa maana hiyo naamini kwamba wote waliochangia walichangia vizuri sasa yaliyobakia ni kurejea rejea tu yale ambayo wamechangia wengine. Kwa hivyo, mimi sitotaka kurejea kwa yale yote waliochangia wenzangu na haswa jana Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu naomba nikupongeze sana kwa mchango wako mzuri pamoja na wengine wote ni wajibu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, mimi nataka kurejea kusoma *Hansard* ya tarehe 5 Aprili, 2011. Baada ya kumaliza maswali na majibu, Mheshimiwa Spika, ulisema hivi: "Waheshimiwa Wabunge baada ya hapo tutaendelea na shughuli zinazofuata Muswada wa Sheria ya Serikali Kusomwa Mara ya Kwanza. Muswada wa Sheria ya Mapitio ya Mabadiliko ya Katiba ya nchi ya mwaka 2011 (*The Constitutional Review Bill 2011*). Muswada huu uliotajwa hapo juu ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza. (Makof)

Mheshimiwa Spika, uliendelea na kusema Waheshimiwa Wabunge huu Muswada umeletwa kwenu na kwa kuwa umeletwa basi sasa tunaupeleka kwenye Kamati ya Katiba na Sheria na wao itabidi wafanye *public hearing* yaani ni kuwaalika wadau mbalimbali waweweze kuusikiliza Muswada huu na kuweza kutoa maoni yao. (Makof)

Mheshimiwa Spika, hii peke yake naomba niwaambie Watanzania wenzangu kwamba jamani Muswada huu ulishasomwa kwa mara ya kwanza na hii ni mara ya pili. Kwa hivyo, naomba

Watanzania tusikae na kusikiliza watu ambao hawatutakii mema katika nchi yetu ambao wanaanda labda fujo au wanataka kulazimisha kwa yale waliyoyaona Zanzibar kwa maana muafaka wa Zanzibar, kati ya Chama cha Mapinduzi na Chama cha CUF basi na wao tutengeneze kama ilivyokuwa vile sasa na muafaka ule uje huku. Kama ni matarajio yao basi waingize tu utakapokuja Muswada ule, utakapokuja, majadiliano yatakapoanza ya Katiba basi waingize yawe mawazo yao halafu watu watapima, wingi wa kura na wataamua. Kwa hiyo, hakuna haja ya kubishana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sitotaka kuchukua maelezo mengi marefu ila naomba, nchi yetu imetulia kwa kipindi kirefu. Kama kuna matatizo ya hapa na pale ni mambo tu ya kawaida wakati mwingine ya kibinadamu kutotaka kuelewa au kusikiliza kwa makusudi. Lakini naomba sana kutumia fursa hii, kwanza niwaombe wananchi wangu wa Wilaya ya Mafia kwanza kabisa maana yake wao ndiyo walionifikisha hapa, niwaombe sana wakati unakuja, yale yote ambayo tunataka kuyajadili na kuyaingiza katika Katiba yetu mpya itakayokuja, basi tutakaa chini na kuweza kuyajadili na kama yatakuwa mazuri basi naamini yatapendekezo mapendelekezo yetu.

Mheshimiwa Spika, yapo mapendelekezo mengi sana ambayo yanazungumzwa. Kwa mfano, huko mitaani watu wanasema kwamba wanazungumzia hata Muungano, huu Muungano bwana una matatizo hapa na hapa, upande mmoja unameza upande mwingine sasa tutakapokwenda kwenye Katiba baadaye tutaweza kuyazungumza ili uwe ufunguo kwa maana uingie ndani ya Katiba yale matatizo yapate kuondoka, ufanوليwe waziwazi ndani ya Katiba. (*Makofii*)

Lakini pia kama alivyosema jana Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, tuna matatizo ya mikataba ya madini, kwa hivyo haya yote yataweza kuingia ndani ya Katiba kama Katiba ya Ghana inavyotamka waziwazi. Lakini pia na sisi Bunge la Katiba kuwa na nguvu baadaye kama vile Mheshimiwa Rais anapoamua kuteuwa Majaji, Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, kabla hawajateuliwa rasmi, waje kudhibitishwa na Bunge, hayo yanazungumzwa, kwa hiyo, Bunge la Katiba litakavyokuja hapa tukiwathibitisha ndipo watakapoweza kwenda kufanya kazi kwa mujibu wa Katiba mpya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini lingine hata nje watu wanasema siwasemi vibaya Mawaziri, lakini watu wanasema wakati umefika Mawaziri wasiwe Wabunge ikingia ndani ya Katiba basi yote haya yataweza kufikiwa na pale ambapo tutaona hapa sasa ndiyo mambo yanafaa. Kwa hivyo, Waheshimiwa wananchi, mnaojiita wanaharakati naomba sana wakati mtakapokaa muangalie mpango mzima, msije mkafanya mambo ya kushawishi kundi la watu waweze kuingia katika fujo na nchi yetu ikaweza kupoteza amani na utulivu iliyokuwa nao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine naomba sana haya yote wanayapata kuitia vyombo vya habari. Vyombo vya habari chonde chonde majadiliano mnayoyaweka, midahalo mnayoiweka na ukiangalia katika baadhi ya vyombo vya habari utakuta mara nyingi kundi lile moja lilitokuwa linakwenda kuzungumza basi kwa kiwango kikubwa linakuwa ni wale wale wanaharakati. Kama mnataka usawa wachukueni wanaharakati wale wale mnaowaalika wawekeni upande mwingine. Lakini wawekeni na watu ambao wanafahamu kwa mfano kwa kuitumia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, tafuteni Wanasheria, nendeni mkawaweke upande wa pili ili wale watakaposema na wale waweze kujibu zile hoja zinazotolewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini mnapowaweka watu kundi moja basi itaonekana wale kama vile mmewapanga na mara nyingi hata katika kipindi fulani ambacho anaongoza Bwana mmoja anaitwa Masako.

Mimi mwenyewe najaribu sana kukifuatilia kila ninapopiga simu kutaka kuchangia utakuta ile simu haipatikani kabisa ipo *busy* wakati mwingine utaambiwa simu unayoitumia haifanyi kazi, ndiyo katika Shirika hili la *ITV*. Wanakwenda vizuri, lakini katika vipindi vile utakuta unapotaka kupiga simu haupati, lakini yeche yule Masako utasikia fulani kutoka sehemu anakuwa keshamjua, keshamtaja na aemeshamtayarisha, maana yake sisi dhana yetu kwamba yule mtu ameshamtayarisha kwa ajili ya kuipiga Serikali. Wanatafuta watu wanaiponda Serikali ili

waweze kuonekana lakini wale watakaosema vizuri hakuna mtu anayeweza kupata fursa hiyo. (*Makofi*)

Sasa tunaomba kama zile *line* labda moja utasema iko *busy* wekeni *line* tatu, nne, tano, halafu na ninyi muwe mnaangalia kama kaongea mwanamme, aongee mwanamke, aongee mtu wa Bara, aongee mtu wa Visiwani. Fanyeni uwiano huo ili kila mtu aweze kuchangia. Lakini siyo wewe mtangazaji ndio unapanga hapa sasa hivi kuna mtu kutoka Moshi, toka Kilimanjaro kutoka Mwanza kutoka maeneo mengine. Inakuwa mnatuchanganya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho mpaka dhana inafikiriwa kwamba naona taabu sana kutamka lakini wakati mwininge tunasema Kituo cha *ITV* naomba vipindi vyenu mnavyoviweka viwe vipindi nya uwazi.

Namba zile mtakazokuwa mmeziweka zitumike wakati wowote, awekwe mtu wa kupoeka ili itakapoingia tu basi aseme subiri sasa hivi anachangia mtu mwininge ili baadaye na wewe utaingia. Lakini ukisema upige *direct* kwa kutokea pale, pale inaonekana ni uchakachuaji ambao unafanywa na wale wanaosimamia vile vipindi. Kwa hivyo, hilo kwa manufaa ya kwao au kwa manufaa ya wale wanaokwenda kuwaita. (*Makofi*)

Sasa naomba sana, sisemi vibaya, wala silisemi vibaya Shirika *ITV*. Najua kibinadamu wanawenza wakajihisi vibaya, lakini nazungumza hilli kwamba watakapofanya jambo hilli liwe la uwazi. Liwe la uwazi na wenye magazeti kwa mfano vyombo nya habari vyote naomba sana kama wanataka kuita midahalo kama wanavyofahya *TBC* vipindi nya asubuhi atachukuliwa mtu mmoja kutoka Upinzani, mmoja Chama Tawala, wakiwekwa pale kila mmoja wanakuwa *wanadeal* na yale mambo na kila mmoja anakuwa anatoa hoja kwa kujenga misingi kwa vile kwa ufahamu wake. (*Makofi*)

Kwa hivyo, hilo ndilo ninalotaka kulisema. Siipigii debe *TBC* lakini naomba kuwapongeza lakini na wao *ITV* waweze kufanya midahalo hii kwa haki na usawa. Sina mengi ya kusema na naomba kusema kwamba naunga mkono hoja hii lakini amani na utulivu ndiyo wajibu wa Watanzania. Kisiwa pekee kilichobakia katika dunia hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni wengine wataalam wangu waliisahau, kuna Watendaji wa Kata 18 kutoka Jimbo la Mheshimiwa Richard Ndassa, wapo Watendaji 18. Poleni sana hawakuwaandika watu wangu kwa sababu ninyi mmekuja wengi kwa lengo la kujifunza. Kwa hiyo, karibuni sana na wanaongozwa na Katibu Tarafa, Bwana Joseph Kazoba. Ahsante sana. Hawa wanatoka jimbo Mheshimiwa Ndassa, karibuni sana na ahsante sana. Mchangiaji anayefuata sasa ni Mheshimiwa John Lwanji.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Awali ya yote nikushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kutusaidia sana sisi Wanakamati katika kukamilisha Muswada na ukaweza ukaletwa hapa. Katika Kamati tuko watu 16 hivi lakini uliona ni busara uongeze watu ili tuweze kuwa na mawazo mapana zaidi na tulifanya kazi hiyo kwa uadilifu na kwa ujasiri wa takribani muda wa wiki tatu hivi na nusu na ndiyo ukaweza kufika hapa. Sasa yote haya tuliyoyafanya tuliyafanya kwa uaminifu kabisa na kwa uadilifu. Hatukuwa na hila, tuliamka kazi nydingi tukawa pale na *concentration* yetu ikawa kwenye Muswada kutoka Dar es Salaam mpaka hapa tulikuwa *serious* Kamati ilikuwa ipo *serious* sana katika kuujadili na katika kuwashirikisha wadau. (*Makofi*)

Kuna wenzetu wachache hawakuwa *serious* lakini tulilliona hilo na halikuweza kutuzuia kufanya kazi. Walifika na kusaini na kwa madhumuni ya kufanya ushushushu ili kujua kinazungumzwa nini na wao wakatoka kwenda kuwasiliana na Wanaharakati nje kwa utaratibu wa kuweza kuvuruga. Lakini kwa bahati nzuri tulismama kidete. Tulifanya kazi hiyo kwa mujibu wa Kanuni Namba 84(2) inayosema: "Kamati iliypolekewa Muswada itatoa matangazo au itatoa barua ya mwaliko kumwalika mtu ye yeyote afike atoe maoni yake mbele ya Kamati hiyo kwa lengo la kuisaidia katika uchumbuzi wa Muswada huo."

Mheshimiwa Spika, haya yote tuliyaafanya kwa uadilifu mkubwa sana na watu walifika na watu waliofika hao wadau walifurahi sana waliona wamepewa heshima na walichangia bila kinyongo na wale ambao hawakufika mbele ya Kamati wao tuliwaomba walete kwa maandishi na wengi walifanya hivyo. Sasa kinachonishangaza ni kwamba kuna watu ambao bado hawajaelewa hii dhana ya uwakilishi kwa sababu Rais amechaguliwa na watu, Wabunge wamechaguliwa na watu, Madiwani wamechaguliwa na watu na tumejiwekea kanuni za kufanya kazi. Sasa tunapokuwa hatuaminiwi katika *stage* hii na kuwapotosha wananchi kwamba sisi ndiyo tunaunda Katiba, imetushangaza sana. Muswada huu hautungi Katiba, Muswada huu tunayarisha kama alivyosema Mheshimiwa Chenge, ni miundombinu ya kuunda Tume ambayo itakwenda sasa kuwashirikisha watu wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nawakilisha Jimbo la Manyoni Magharibi, kule wananchi wanausubiri Muswada, wanausubiri Tume kwa hamu kubwa sana kuja kutoa maoni yao. Watu wa Itigi wanausubiri Tume, watu wa Kata ya Majengo wanausubiri Tume. Watu wa Iludyandole wanausubiri Tume, watu wa Sanjaranda wanausubiri Tume, watu wa Mgandu wanausubiri Tume, watu wa Mitundu wanausubiri Tume, watu wa Rungwa wanausubiri Tume na Mwamagendo wanausubiri Tume. Wote hawa wamenieleza mimi mwakilishi wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa itakuwa ni ajabu sana unaponivua dhana ya uwakilishi wa watu hawa. Maana sasa wengine wanakwenda *ina-ball down* kana kwamba mimi ninapowakilisha hawa watu 170,000 basi wengine wanafikiri kwamba basi tuwaweke kwenye mabasi wale watu 170,000 waje hapa zamu hii iwe labda ya leo iwe ya watu wa Manyoni, kesho iwe zamu ya watu wa lleje, iwe zamu ya watu wa Chilonwa. Kweli itawekezana Mheshimiwa? Kwa sababu vyombo tumeshaviweka, ni lazima tuvitumie. Sisi tupo hapa tunawawakilisha hao wananchi. Sasa suala ndiyo hilo kwamba huu Muswada urudishwe tena wakati yale yote tulyokubaliana yamefanyiwa kazi na tena umerekebishwa, umetafsiriwa kwa Kiswahili ili waweze kuuelewa zaidi. Hatuwezi kwenda mbele zaidi ya kitu tulichokifanya. Hiyo itakuwa ni kuingilia kazi ya Tume sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni lazima tufikie hatua ya kwamba ni lazima tuainishe mipaka, sisi tumefanya mpaka hapa. Bunge hili limefikia linauridhia Muswada huu. Sasa Rais achukue hatua Tume iundwe. Tume ndiyo ipite kila mahali kwenda kuwahoji wananchi. Hao watu niliowataja wanawasubiri. Tulichukua sampuli ya watu wa hapa Dodoma wakati uliposomwa Muswada kwa mara ya kwanza halafu tukaenda Zanzibar halafu na Dar es Salaam ilitoshya kabisa maoni hayo. Sasa Tume itakuja, itapita sehemu zote na wadau wengine walipewa nafasi katika vyombo vya habari na watu wengine wakawa wametoa maoni. (*Makofii*)

Kwa hiyo, mimi sioni sababu yoyote ya kuupigia kelele katika hatua hii. Dhamira ya Rais ni nzuri katika Muswada huu. Nashangaa kwa nini hawamwamini katika Kamati hiyo tulikuwa tunawaona watu wengine kanakwamba wamekuwa *allergic* wakiona lile jina Rais basi anastuka. Tunashangaa maana nayo nakumbuka wakati Rais anaingia madarakani kwa mara ya kwanza mwaka 2005 kati ya mambo aliyokuwa ameahidi kwamba ange-resolve ni suala la muafaka wa Zanzibar hawakumwamini watu wengine lakini hilo suala leo lipo wapi suala la muafaka wa Zanzibar. Limekuwa *resolved* na watu wako katika hali shwari kabisa. Kulikuwa na mgogoro na mvutano sana mustakabali wa Zanzibar. Lakini kwa nia yake nzuri akawa amelifikisha hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeomba kwamba tusonge mbele wala tusirudi nyuma, tuupitishe Muswada huu uende kwa wananchi sasa wakafanye kazi, sisi tuliwashirikisha. Hata Jukwaa hilo la Katiba huyo bwana alikuja katika Jukwaa la Katiba ambaye anapiga kelele sasa hivi alisema wazi kabisa ye ye anawakilisha Taasisi 150. Sasa kama anawakilisha Taasisi 150 sasa anacholaamu ni nini maana wamemtuma. Hatuwezi kuita Taasisi 150 zikaja kwenye ukumbi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nadhani tusikose uzalendo katika suala hili, tusije tukaugua ugonjwa wa kukosa uzalendo, itakuwa ni mbaya. Mimi mawili tu niliyoyaona katika Muswada kuhusu suala la gharama, gharama hizi za Tume na gharama za Sekretarieti naona zimeanzishwa lakini iko *silent* katika zile gharama za Bunge la Katiba, hapo labda ingeweza kuangaliwa. Halafu kuna *rigidity* katika suala la hadidu za rejea, zimeingizwa kwenye Muswada lakini niliona kwamba inaweza kuja

kuwa ngumu wakati Tume inafanya kazi. Kwa hiyo, nilidhani kwamba ingekuwa vema hizi zingewekwa kwenye Jedwali ili iweze kuwa na *flexibility* kwamba kama kunatokea na tatizo, basi Waziri mwenye dhamana ashirikiane na watusika waweze kufanya *amendment* ndogo ndogo ili Tume iweze kufanya kazi zake bila tena kikwazo chochote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, vinginevyo inaweza kuleta mgogoro au matatizo na si rahisi kuliitisha Bunge tena kuja kushughulikia jambo hili. Kwa hiyo, hilo naomba liweze kuangaliwa. Kwa kifungu hatuwezi kuendesha mambo kiholela, ni lazima tuwe na utaratibu. Nilipokuwa mwanafunzi alikuwepo Mhindi mmoja alikuwa akipita mashulenani anaendesha michezo hii ya kiini macho. Sasa alikuwa anatumia neno anasema *brakadabra brakadabra*, sasa akifanya kitu unaona kichwa kama vile mazingaombwe. Lakino hilo kwa tafsiri ya Kiingereza inasema *a word that people say who when they will do a magic trick in order to make successful*, ndicho kinachofanyika hapa kwa wenzetu hii ni *brakadabra*, ni *brakadabra* hakuna kitu kingine kinachofanyika hapa, ni kiini macho tu. Sasa inapofikia hatua ya kwamba Serikali inafanya mambo mazuri basi watu wanaona kwamba hiyo si vizuri wanataka kila wakati tuharibikiwe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, basi hatuwezi kwenda mbele, kitu kizuri kitoke kwao. Tuna vikundi vinavyotaka kwamba wao mawazo yao yote yachukuliwe, *you win all*. Sasa haiwezekani, mawazo na dini lazima vitakuwepo, watu wana maoni mbalimbali na ndicho kitu tumefanya hapa. Kwa hiyo, hatuwezi kuwa na vimchezo kama hivyo ninavyosema vya *brakadabra* kiini macho kuwadanganya wananchi na kuwapotosha wananchi haiwezekani hata kidogo. Na naomba kwa hili Serikali iwe makini, nawasikitikia sana wa upande wa wenzetu kwa kujiingiza humo na mimi ninavyoona wameingizwa na mtu mmoja, wawili. Sasa hivi wengi wanajuta tu. Kwa sababu wananchi wameshaelewa. Mchezo huu na hawawezi kuuchenza huo mchezo. Huo mchezo ni kiini macho. Sisi hatuwezi ku-*entertain* vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, watu wenge busara zao wamekaa Mheshimiwa Mzee Mrema yupo hapa anasikiliza kama ana hoja anachangia hapa. Mawazo mbalimbali tulipata kutoka upande wetu wa *CUF* akina Hamad Rashid Mohamed, ni watu wenge busara walitusaidia sana. Sasa hawa watu wengine basi wananchi watawapima, watawapima na watatoa hukumu yao waone kabisa siku hiyo watu watoke kwa wingi, watoe maoni yao basi ili tuweze kuja na Katiba ambayo itatusaidia. Watu wana matatizo yao wanataka wayarekebishe katika Katiba. Sasa kama tulitaka siku 100 wanasema wao watafanya siku 100 sasa sisi tunakwenda kwa utaratibu na tumekubali na tupo katika *train*, katika reli sahihi. Sasa hatuwezi watu wachache waweze kutu-*delay*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mimi nakushukuru wewe binafsi, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Lakini watu wangu hao ninaowawakilisha, wapo tayari, wao wanasubiri Tume, wametuamini, mimi wameniamini wamenileta hapa. Wamesema bwana hebu katusikilizie na habari nzuri mimi najivunia kwamba naandika historia nikiwa kama Mwanakamatii kushiriki katika jambo hili muhimu sana la Kitaifa. Mimi itabaki kama historia hata kama nitakufa lakini jina langu litabaki katika vitabu hivyo kwamba nilishiriki katika mchakato huu muhimu sana. Hatujui ni lini tena kitu kama hiki kitakuja kutokea. Kimetokeea baada ya miaka 50 na ime-*concede* vizuri sana na wakati huu wakati ambapo tunaadhimisha miaka 50 Uhuru. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mimi niishie hapo na ninasema wazi tu kwamba ninaunga mkono hoja. Mahali ambapo mimi huwa siungi mkono hoja nasema wazi tu, uongo kweli ndugu zangu? Nasema wazi kabisa kwamba mimi, lakini ninasema wazi, huwezi magwiji kama akina Mheshimiwa Ole-Sendeka wote tuliwashirikisha Waheshimiwa wapo watu mahiri maana ni lazma tukubali kuna watu mahiri kwenye *field* fulani. Vinginevyo tutakuwa hatueleweki kama mtu anajitokeza na utaalam wake tunautumia vizuri na tulitumia vizuri sana *experience* za Waheshimiwa akina Mzee Chenge na watu wengine na hatukulala. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof!*)

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mtera niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mimi kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kutufikisha salama siku ya leo. Zaidi sana nikushukuru kwa namna unavyoliendesa Bunge letu kwa umahiri na umakini na kufuata Kanuni zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nianze tu kwa kuzungumzia Serikali yetu. Tumesikia hoja nyinyi zikisemwa hapa Bungeni na Wabunge na wengine wakiwakejeli Mawaziri wetu kwamba wanalala. Wengine wakiwakejeli Serikali yetu kwamba legelege, tunataka tuone ulegelege wenu katika jambo hili. Jambo hili si jambo la kuchezewa. Kuna mtu mmoja sijui Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba, ameipa Serikali siku 30.

Mheshimiwa Spika, mimi nasema siku 30 ni nyinyi, angepunguza! Angepunguza ziwe siku tano au kumi, halafu tuone yeche anataka kufanya nini na Serikali inasema nini. Katika mambo ya msingi tusikubali kutishana, hii nchi ni yetu wote, sio nchi ya mtu mmoja hii. Habari ya kugeuza siasa kuwa mambo ya udalali wa kutafutia fedha za wafadhili, ni kitu ambacho kitaliangamiza Taifa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza mimi nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Tundu Lissu, tofauti na wenzangu wengi. Mheshimiwa Tundu Lissu, ameonesha kilichoko moyoni mwake na kilichopo kwenye miyo ya wenzetu kuhusu Muungano wetu. Ameonesha kwamba wao hawako tayari, ameonesha dharau kubwa na matusi makubwa kwa Wazanzibari. Kwa hiyo, hata Wazanzibari waliopo CHADEMA, wapo kwa kujipendekeza, wale wachache waliopo wanajipendekeza tu! Wenzao wanawatazama kwa mtazamo ule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na hii dharau ya kudharau sijui huyu kashinda kwa kura chache, sijui huyu, aah! Mheshimiwa Tundu Lissu, kashinda kwa kura 1,700! 1,300 sijui 1,200! Sasa mtu aliyesinda kwa kura 1,700 anabeza mtu aliyesinda kwa kura 30,000 anabeza mtu aliyesinda kwa kura 3,000! Unajua ukijiunda kwa dharau sana, mwisho wake unajikuta unajidharau hata wewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia Muswada huu ambaeo ni hoja ya msingi katika uundaji wa Katiba: nawasikitikia sana Wabunge wengi ambaeo mtu anahutubia, nipo tayari kufa kwa ajili ya Katiba, wewe huna watoto! Mimi siko tayari kufa na Katiba Mpya naitaka. Tusitishane kwamba wewe upo tayari kufa! Unamtisha nani? Kama upo tayari kufa, wewe kufa tu lakini usiliuwe Taifa kwa sababu, eti mfadhilli atakunyima hela. Kuna watu wamezungumaza hapa hoja za ubinasi, wamezungumza Serikali za kidikteta, wamezungumza upendeleo! (*Makofii*)

Mimi hapa nataka kuwa wazi. Hii nchi ni yetu wote na sisi wengine wala hatujali kutukanwa, wengine wameanzisha mitandao ya kutukana watu. Mimi wala sijali, hakuna tusi jipya mtu atanitukana. Hakuna watu wabinasi katika nchi hii na watu wanaoweka viongozi kwa unasaba kama CHADEMA. Katika Viti Maalum Wabunge 11, Mheshimiwa Tundu Lissu ana dada yake kwenye Bunge hili, Mheshimiwa Ndesamburo ana mwanawewe na mkwewe kwenye Bunge hili, nani hajui! Sasa ubinasi ni upi kuliko huo? Wabunge 11, unaweka wanasaba watu nane! Wewe huoni kwamba hapo tunakwenda kubaya? Kwa hiyo, ni lazima tupeane ukweli hapa. Ingekuwa CCM ingekuwa ndio hoja ya kila siku hiyo! Angalia CCM fulani, mtoto wa fulani! Watu wana ndugu zao watu wamejipanga; Mwenyekiti mkwe wa muasisi wa chama, tunajua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunataka tuseme kwamba kama kuna watu wabinasi na watu wanaoweka viongozi kwa unasaba ni wenzetu! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hii habari ya kupita wanatutishia ooh, sijui hii Serikali ya ukoo, sijui Serikali ya kinasaba! Wao ndio wangeunda Serikali ya kinasaba; Viti Maalum 11 wamewewa ndugu kibao! Mzazi mwenzake Katibu Mkuu, yumo kwenye Bunge! Mzazi mwenzake Mkama yupo humu kuititia CCM? Mbona tunataniana jamani tuseme vitu vya ukweli, jambo la msingi hapa ni kwamba kuna wenzetu wanafadhiliwa na nchi za nje wakiwemo Wajerumani, waliwaahidi wakawaambia mkifanya vurugu katika jambo hili la Katiba, tutawapa fedha. Sasa tumewakata maini kwa kulianzisha kwa amani, ndio maana jamaa wanakimbia! Wanajua watasema nini kule! Wanataka usomwe kwa mara ya kwanza ili wapate muda wa kuendeleza vurugu! Hii habari ya

kuwasih i watu wasiandamane jamani, tuiache! Waacheni waandamane na weny e kuzuia nao wapo. Hii habari ya kusema tunawasihi, tunawasihi, tunawasihi nini? Hakuna sababu ya kumsihi mtu, wanaotaka kufanya fujo wapo na wanaozuia fujo wapo kwenye nchi hii, shida iko wapi? Hapa hakuna sababu ya kusema tunakaa kwenye Bunge, tunawasihi! Mimi nataka niwaambie wananchi wa Jimbo la Mtera, kama wapo wanaotaka kufanya fujo wafanye kwa sababu na wanaotaka kuzuia fujo nao wapo tayari. Mwenye masikio na asikie. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika jambo hili tusianze kufuata ubabaishaji, hapa kuna watu wanafanya udalali wa kisasa, wanatafuta hela kwa wafadhili, wanajua *gap* hii ikizuiwa ikaenda kwa amani na utulivu na tukaijadili kwa utaratibu italeta shida. Huwezi ukaanzisha kitu kwenye nchi kama hii yenye Rais, yenye kila kitu, halafu ukamuondo Rais! Yaani ni kama vile tunafanya mapinduzi sijui ya kisasa, halafu tukasema Jukwaa la Katiba ndio liteue Tume! Aah! Litapata wapi Bajeti? Litapata wapi *mandate*? Watapata wapi nguvu za umma za kwenda kuzungumzia jambo hili? Kwa hiyo, tuisitishane kwamba eti mtu ana watu! Kila mtu hapa ana watu ndio maana kaja hapa, hakuna mtu aliyejileta kutoka nyumbani kwake! Hivi ni vitisho tu hivi, danganya toto tu hapa, tunatishwatishwa, tunababaishwa na vitu ambavyo wala havina maana yoyote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwenye suala la kuupitisha Muswada huu mimi nataka niunge mkono kabla sijamalizia maana nisije baadaye nikajisahau, naunga mkono hoja. Lakini nataka nizungumze kuhusu uhuru wa mtu kutoa maoni. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tulisema tangu mwanzo; mwanzoni wakati wenzetu mnaleta hoja hii ya Katiba Mpya, sisi tulisema bora ingekuwa ya mabadiliko ya Katiba kwa sababu, Katiba yetu inatamka mipaka ya Tanzania. Huwezi ukaanzisha Katiba ambayo itabadii mipaka ya Tanzania kwamba hatupakani na Uganda hatupakani na Kenya! Kwa hiyo, kama kuna vitu vya nyongeza, tuviongeze; wakasema aah, tunataka mpya. Tukajua mpya wakati mwingine jina, maana siku hizi Tanzania ukisikia Mzee usifkiri umri, wapo wazee vijana ni jina tu, anaitwa Mzee. Kwa hiyo, sisi tukasema kwa kuwa wenzetu hawa wanataka neno mpya liwepo basi tuweke neno mpya, tusigombanie neno. Lakini ukweli ni kwamba ni marekebisho ya Katiba; huwezi kutunga kitu kipy! Hata ukitunga kitabu kipy cha dini, lazima kitakuwa na mahusiano na *Quran* na kitakuwa na mahusiano na Biblia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo leo Watanzania tuisidanganywe hapa kana kwamba eti tukiandika Katiba Mpya, mvua ndio zitanyesha sana, sijui ndio baisedhi hazitapata pancha! Katiba ni Sheria mama tu. Tuisidanganyane hapa, tuisidanganyane hapa, hatuwezi kuandika katiba iliyopita Biblia na *Quran*, tuisidanganyane! Kama ni uadilifu tungefuata vitabu vya Mwenyezi Mungu. Na hili la Katiba sio suala la wanasiisa! Viongozi wa dini wanakaa kimya! Mimi nataka niwaambie, chama chetu tunalo Baraza la Wazee, wakati mwingine tukikengeuka linatokeza linatuonya. Lakini wenzetu chama chao kinangojea mpaka Mheshimiwa Zitto, agombee uenyekiti, ndio chama kinamuita! Aah, toka, ni nafasi ya mtu fulani! (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi hapa David Cameron kazungumza mambo ya kitoto hapa! Anatupa masharti ya ajabu! Sijaona Baraza la Wazee likisema. Vijana wao wanafanya fujo wanaharibu hali ya hewa ya nchi, wamekaa kimya! Hivi hawa wazee wa CHADEMA wao wana sehemu ya kukimbia hii nchi ikiingia vurugu! Ni lazima tuambizane ukweli hapa kwamba tupo hapa kwa maslahi ya nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali, nataka niwashauri hili jambo, mwakani tuna sensa, sensa itachukua zaidi ya shilingi bilioni 500 na zaidi. Lakini ukija ukiingiza suala la Katiba, nalo litachukua zaidi ya shilingi bilioni 600 na kitu! Ukiingiza uchaguzi wa Serikali za Mitaa, nao unachukua mapesa chungu nzima! Uje Uchaguzi Mkuu, unachukua ma-trilioni ya pesa! Tutashindwa kuwanunulia Watanzania dawa. Tukiona hili jambo hatuwezi kwenda na mambo makubwa yote kwa wakati mmoja, uchaguzi wa mwaka 2015 tuuahirishe, tuunde Katiba inayotakiwa na Watanzania, tumuongezee Jakaya Kikwete miaka miwili ya kuunda Katiba ili kila Mtanzania aweze kutoa maoni yake, mwaka 2017 tunafanya uchaguzi. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kwenda na mambo matano haya yote ukafanikisha bila kuangusha uchumi wa nchi, maana hivi vitu vyote vinachukua pesa, havilingizi. Na huduma za Watanzania zinatakiwa! Suala la Rais kutoa hadidu rejea, linawasumbua wenzetu wachache; hadidu rejea, Rais ni Taasisi, sio kwamba Rais atakaa pale aandike yeye. Wataandika, watampelekea, atatoa *comment* zake na kuna vitu miiko, ni lazima tuizingatie! Tanzania sasa tumeacha miiko, tumeacha nidhamu! Tangu tumefuta viboko kwenye shule za msingi, tumetengeneza kizazi kibaya sana katika nchi hii. Kila mtu anajiona anaweza kusema wakati wowote na mahali popote, kitu ambacho sio sawa! Kuna vitu vingine ilikuwa ni mwiko kuvizungumzia! Leo kuna watu wanatoa kauli ambazo zamani tungeziita ni za uhaini! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia Muungano kwa lugha ambazo zinazungumzwa humu, zamani ungekuwa ni uhaini moja kwa moja. Unapozungumzia madaraka ya kumuondoa Rais kwenye nafasi yake ukajiweka wewe pale! Hivi jamanii, ndio maana hata Mungu hakutaka tukae nae kikao, alijua kisingeisha! Wengine wangesema mvua hawaitaki, wengine wangesema jua hawalitaki! Mungu akaamua tu mvua itanyesha kwa wakati atakaoutaka yeye, jua litawaka kwa wakati atakaoutaka yeye! Mbona hawazungumzi? (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hatuwezi kuwa na nchi ambayo kila mtu ana sharubu! Hapa mwenye sharubu ni mmoja tu, Jakaya Kikwete! Na ndio tunayemsikiliza, hatuwezi kusikiliza watu wengi! Tunamsikiliza Rais mmoja wa nchi yetu. Na hayo madaraka tunayotaka kuyapunguza sio ya Rais huyu, ni ya Rais ajaye! Huyu anayo tayari. Maana wengine wamejisahahu wanafikiru tunataka tumpunguzie madaraka Rais Kikwete, aah! Huyu ameshaapa kwa mujibu wa Katiba hiyo ambayo na sisi tumeapa tutailinda, madaraka yote *full* anayo; kama tunataka Rais wa Tanzania awe na nguvu kama Mjumbe wa nyumba 10 ni huyo ajaye, sio huyu wa sasa hivi. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Haya, tunaendelea. Kama uliapa kwa Katiba hii, uchaguzi wako ni mwaka 2015 na sio vinginevyo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, atafuatiwa na Mheshimiwa Benadertha Mushashu.

Hayupo! Mheshimiwa Benardetha Mushashu.

MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye Muswada huu. Kwanza kabisa ninampongeza Mheshimiwa Waziri, Mwanasheria Mkuu na Kamati, ambao wameweza kuandaa na kuendelea kuboresha Muswada huu, kwa kadri walivyoendelea kupata mawazo ya wadau mbalimbali. Kwa namna ya pekee nampongeza Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ambaye amewasikiliza Watanzania wanataka nini na akaridhia kwamba sasa huu mchakato wa kuweza kuelekea kutengeneza Katiba Mpya uweze kuanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utakuwa na maeneo makuu mawili. La kwanza, nitajikita kwenye vifungu mbalimbali, lakini la pili nitazungumzia juu ya upotoshaji unaoendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukiungalia huu Muswada, kwanza Muswada wenye umechapishwa kwa Kiswahili, ambalo ndilo lilikuwa pendekeso la Watanzania walio wengi. Kwa hiyo, ina maana kwamba Watanzania wengi watausoma na kuweza kuulewa.

Mheshimiwa Spika, lakini ninachoiomba Serikali ifanye sasa, ili kuhakikisha kwamba wanaondoaa upotoshaji, elimu ya aina mbili itolewe; kwanza, watu waeleweshwe ndani ya Katiba iliyopo kuna nini, lakini la pili ni huu mchakato wenye, kwa sababu ni mpya kabisa haijawahi kutokea katika Tanzania, kwa maana ya kushirkisha Watanzania wote, tuelewe kila mchakato, kila *stage* ya mchakato huu ina maana gani na Mtanzania anatakiwa kufanya nini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikianza na sehemu ya kwanza. Sehemu ya kwanza ambayo inazungumzia juu ya tafsiri, Ibara ya 3; Ibara ya 3 inasema Mabaraza, maana yake ni mikutano, mikusanyiko, hadhara au majadiliano huru na ya wazi yaliyotayarishwa au kuandalisha na Tume kwa madhumuni ya kukusanya maoni ya wananchi juu ya rasimu ya Muswada wa Katiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiisoma hiyo pamoja na Ibara ya 16(6), (7), (8) na (9) kinachoeleza juu ya Mabaraza haya ni kwamba Mabaraza ya Katiba yataundwa na Tume kwa muda maalum, kwa kuzingatia mgawanyiko wa kijigrafia wa Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile pale chini kilichonifurahisha ni kwamba yatahudhuriwa na raia wa Tanzania pekee. Maana yake ni nini, kwamba sasa sisi baada ya huu mchakato wa huu Muswada tunaouandaa, Tume itakapoundwa itaenda kwa wananchi, itakusanya maoni, itaandaa rasimu. Lakini hii haitakuwa mwisho, hiyo rasimu itakayokuwa imeandalisha watachapisha kwenye magazeti, wananchi wataangalia je, maoni yao waliyoyatoa yamo? Na kama yamo, yameandikwa namna gani? Baada ya kuchapishwa sasa wananchi wamesoma, wameelewa kilicho kwenye rasimu, Tume itarudi kwa wananchi, itafika hata kule kwetu Kaisho, Kanyigo, kule Rulenge, Muleba pale, wataenda kuongea tena na wananchi katika makundi mbalimbali wakizingatia hali ya jijigrafia katika Mabaraza hayo; *Constitutional Conferences* katika haya Mabaraza sasa Watanzania tutakuwa tumepewa nafasi nyingine ya kurekebisha na kuboresha tena rasimu ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, baada ya wananchi kuweka mawazo yao, ripoti vilevile itaandikwa na hii Tume na baada ya ripoti kuwa imeandikwa itaendelea na mchakato wa kwenda kwa Rais na badaye itaweza kutufikia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kuongea hapa naomba katika Mabaraza haya yatakayoundwa, yaweze kushirikisha makundi mengi zaidi, yaweze kushirikisha watu wengi zaidi ili kama yanavyotamkwa huku kwamba yatakuwa huru, yatakuwa wazi na yatakuwa shirikishi. Lakini ningependekeza kwamba katika *stage* hii kama nilivyoosikia wengine wanapendekeza, Mabaraza haya yasihusishe vyama vya siasa, tutavuruga ndugu zangu! Hii *stage* ni mapema mno kusema kwamba Mabaraza haya yaundwe na vyama vya siasa.

Mheshimiwa Spika, hebu tuangalia kilichotokea Kenya, Kenya walipofikia *stage* hii, wao Mabaraza yao yaliundwa na vyama vya siasa. Lakini kilichotokea ni kwamba mlisikia *Bomas One*, ikashindikana, *Bomas Two* ikashindikana, *Bomas Three* ikashindikana mpaka Rais alipoona kwamba ili Muswada huu uende akaamua kwamba aunde Tume mambo yakaendelea mpaka wakapata Katiba. Ninapenda nishauri kwamba kama utaratibu ulivyoandalisha humu uende hivyo hivyo, kusudi sisi wanasiasa na vyama vyote vya siasa vitakuwa vimewakilishwa kwenye Bunge la Katiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Ibara ya 19 inayozungumza kwamba mtu atakayekwamisha na kumkwaza au kumzuia Mjumbe wa Tume au Sekretarieti kutekeleza majukumu ya kutekeleza mamlaka ya Tume au Sekretarieti, atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa kulipa faini isiyozidi shilingi milioni tano au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi 12. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napendekeza kwamba kwenye kipengele hiki kingeanza kusomeka kwamba: "Mtu ye yeyote atakayepotosha au kutoa elimu ya kupotosha..." halafu iendelee; kwa sababu naona kuna watu wengi watafanya hivyo watapotosha, halafu wataharibu. Kwa hiyo, naomba na wao waingie mle kusudi waweze kushughulikiwa na kifungu hiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge ni wawakilishi wa wananchi na wote hapa tupo ndani kwa ridhaa ya wananchi, watu wanachotaka, Watanzania wanataka Katiba. Wametutuma tuje tukae humu ndani, tujadili, lakini mwisho wa siku baada ya mjadala na mchakato mzima, wapate Katiba wanayoitaka. Nawapongeza Wabunge wa Kambi ya Upinzani wa vyama vya CUF, TLP, NCCR

Mageuzi, nina uhakika na UDP angekuwepo angekuwa hapa, kwa ukomavu wao wa kisiasa na kwa jinsi walivyokubali kujadili mambo magumu na mazito ya Taifa hili. (Makof)

Mheshimiwa Spika, Wabunge wa CHADEMA walizira, wakaondoka humu ndani na sikushangaa kwa sababu wamezoea kuzira. Mimi ninajiuliza na ninawauliza Watanzania huko wazazi; ukiwa na watoto wanne, watano, sita hivi, mmojawao kila ukimsema ni kuzira, ukitaka kuongea nae ananuna, ukitaka kufanya hivi anakataa kula! Unamuachia hivi hivi au unamchukulia hatua unamrekebisha? (Makof)

Mheshimiwa Spika, naomba niulize hawa kwa uzoefu, Waheshimiwa wenzetu wa CHADEMA kila tukianza kujadili mambo mazito, wanaondoka humu ndani! Ningependa kujua, wanaondoka wakiwa wanatumia Kanuni gani kwenye Kanuni za Bunge? Na kama hiyo Kanuni ipo, ni kwa nini hawachukuliwi hatua? (Makof)

Mheshimiwa Spika, mimi kwangu naona hizo ni fujo, wanawalaghai wananchi kwamba wao hawakutoa maoni wakati Mheshimiwa Tundu Lissu, alisimama pale akasoma maoni ya Upinzani, lakini Watanzania ni waelewa wanajua kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, na ukiusoma kwa ndani ule mchango wao, unachochea vurugu, unachochea kuvunjika kwa Muungano. Lakini sisi Wabunge wote tulio baki humu, kwa niaba ya Watanzania wengi walio nyuma yetu, tunasema Muungano hauvunjiki, tutaulinda kwa nguvu zetu zote. (Makof)

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 6 ya Muswada huu inasema kwamba Rais baada ya kushirikiana na kukubaliana na Rais wa Zanzibar, atateua Wajumbe wa Tume. Madaraka haya ya Rais anapewa na Katiba.

Ukiangalia ibara ya 33 inasema Rais atakuwa Mkoo wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi. Wale wanaohojo madaraka ya Rais, wengi mmeshachangia, ni kwa sababu Rais amechaguliwa, wote tulikuwa kwenye uchaguzi Mkoo, huyu huyu ndiye kipenzi cha Watanzania, kwa hiyo, anayo madaraka hayo. Lakini vile vile Katiba inampa madaraka kwa kuwa yeche ni Mkoo wa Nchi. Kama tunataka kutengeneza Katiba mpya au tunataka Tume itakayoanzisha mchakato huu, ni nani anayeweza kufanya kitu kama hicho kama siyo Rais. Kwa hiyo, inabidi tumwamini, tumheshimu tumwache achague tume na tume hiyo iende kwa wananchi kusudi waweze kutoa maoni ya kuweza kutengeneza Katiba mpya wanayoitaka. (Makof)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna upotoshaji mkubwa sana unaendelea wanawalaghai wananchi, wanataka kutujengea chuki kati yetu na wananchi, wanasema tumejifungia humu ndani tunatunga Katiba, lakini si kweli kwa sababu ukiangalia ibara ya nne ya Muswada tunaoutunga, inasema madhumuni ya Sheria yatakuwa ni kuweka utaratibu wa kuunda Tume itakayokusanya au kuratibu maombi ya wananchi na pili kuweka utaratibu ambao utaruhusu wananchi kushiriki kwa mapana katika kutoa na kuwasilisha maoni yao kuhusu Katiba. Sasa badala ya kuwaeleza haya wanawadanganya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nilisikitika sana juzi wakati nilipoangalia mdahalo uliokuwa unaendelea Dar es Salaam, mtu mmoja anainuka anasema wao wanatangaza maandamano baada ya mwezi mmoja watakuwa na maandamano mfululizo yasiyokuwa na kikomo na anathubutu kusema kwamba hawatafanywa kitu chochote *as if* Serikali imekwenda likizo. Tunataka kumwambia Serikali ya Chama cha Mapinduzi ipo na wakijaribu watakiona, tunaomba kama wanataka kwenda kutoa elimu, watoe elimu sahihi lakini wasiwaposhe wananchi. (Makof)

Nasema hivyo ndugu zangu, hebu angalia Arusha, Arusha ulikuwa ni mji wa amani tena ni mji wetu wa Utalii, watalii wengi wanafikia Arusha, hebu angalia kinachoendelea sasa hivi, Arusha imekuwa ni maandamano kila siku. Hebu twende Mwanza, mimi ni mkazi wa Kagera kila siku napita Mwanza, juzi nilikuwa Mwanza, barabara karibu zote zikafungwa watu wanakimbizana na mabomu ya machozi na *who is behind this*, jamani niwaambie Libya walianza hivi hivi, Libya walianza na maandamano ya amani wameishia wapi? Gaddafi ameuawa lakini sasa hivi wao

wanauana wao kwa wao na silaha zimezagaa kila mahali hiki ndiyo tunachokitaka Watanzania ndugu zangu.

Mheshimiwa Spika, nafikiria kwamba, niyaseme hayo kwa sababu naamini kwamba Muswada unaotungwa ni mzuri utashirikisha wananchi katika hatua zote, utakuwa wazi kwa kila stage watakayokuwa wanamaliza, maoni yanarudishwa kwao, yanachapishwa kwenye magazeti, siyo gazeti la Serikali tu na magazeti ya kawaida, watu wanasoma, wanaongeza maoni yao, *at the end of the story* tutakuwa na Katiba nzuri na ambayo kila Mtanzania ameingoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Anna Abdallah na Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale na Mheshimiwa Vita Kawawa wajandae.

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nianze kabisa kwa kuunga mkono hoja hii iliyo mbele yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwaka huu tunaadhimisha miaka 50 ya uhuru wa nchi yetu, ni umri wa mtu mzima, nimemsikia Mheshimiwa Shah anasema yeye ana miaka 50, ndiyo kusema wakati wa uhuru alikuwa mtoto au alikuwa hajazaliwa labda ama ndiyo ametoka kuzaliwa, ni umri mkubwa miaka 50. Mimi wakati wa uhuru nilikuwa na miaka 21, kwa hiyo, najua ninachokisema na nilikwenda kwenye sherehe za uhuru tarehe 9 Desemba, 1961. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika uhai wa binadamu yako mambo muhimu ya mtu kuyakumbuka; kwanza, kuzaliwa kwake, vilevile kama ni mwanaume au mwanamke kuna kuoaa au kuolewa ni mambo ya kukumbuka kabisa, kupata mtoto wa kwanza ni mambo ya kukumbuka katika maisha ya binadamu, lakini mwisho kufa hayo ni mambo muhimu. Katika uhai wa nchi yako kuna mambo ya kukumbuka vilevile. Sisi katika uhai wa nchi yetu tunaanza na kumbukumbu ya uhuru. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tangu tupate uhuru, iliandikwa Katiba ya uhuru, wakati ule wakati wa uhuru tulikuwa watu milioni sita tu, kwa hiyo sasa hivi tuna watu milioni 42 au 45, ndiyo kusema zaidi ya robo tatu ya Watanzania hawakuwepo wakati wa uhuru, hawakujua nani ameandika ile Katiba ya uhuru, hawajui hata kikao cha kufikiria uhuru wa Tanganyika walikaa wapi, hawajui mpaka wasome historia, sisi wengine tulikuwepo, tunaijua.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata uhuru tumeendelea na michakato mbalimbali ya nchi yetu mpaka tumekuwa na Muungano, lakini nafasi ya kuandika Katiba kwa watu milioni 45 walio wengi ni hii ya kwanza watakayoipata baada ya sheria hii kupita, ni nafasi ya kwanza katika maisha ya Watanzania wengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nashangaa kwamba Watanzania hao milioni arobaini na tano, eti hawataki kushiriki katika mchakato lakini hayo ni maneno ya wachache wanaowasemea Watanzania, najua Watanzania wanataka kushiriki mchakato wa Katiba hii tangu mwaka huu mpaka tutakopomaliza huo mchakato. Hili ni jambo ambalo kila Mtanzania ana haki ya kujivunia katika maisha yake kwamba ameshiriki kuandika Katiba. Pamoja na kwamba nilikuwa na miaka 21 wakati wa uhuru sikushiriki kwenye mchakato wa kuandika Katiba, sikushirikishwa kwa sababu lilikuwa ni jambo la kudai tu uhuru, ni harakati zile za kudai uhuru lakini hii siyo harakati tunayoifanya sasa, mtu wa miaka 50 ni mtu mzima, mambo mengi yamebadilika katika maisha yetu, tumeaita mambo mengi ya kisasa, tulikuwa na Vyama Vingi, tukaja kwenye Chama Kimoja na sasa tumerudi kwenye Vyama Vingi, kwa hiyo, ni lazima tuwe na Katiba ambayo leo sisi milioni arobaini na tano tutaiandika ambayo iishi kwa miaka mingine mia moja, hakuna tena kuandika, Katiba haiandikwi kila wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi tuna bahati kwamba, tumeona katika maisha yetu mchakato wa kuandika Katiba na nina hakika Mungu atatupa rehema tutaona mpaka mwisho wa mchakato huu na tutaiona hiyo Katiba mpya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunaposema tunataka kuandika Katiba mpya siyo kwamba leo hakuna Katiba, ipo, hiyo hiyo Katiba ya leo ndiyo inayotupa sisi uwezo wa kusemea Katiba mpya itakayokuja, Katiba hii ndiyo iliyotufikisha hapa Bungeni na sisi wote hapa tuloko humu ndani na Wabunge walio nje ya Bunge ulituapisha ulituapisha wewe na tuliapa kuiheshimu, kuitii Katiba ya leo tulionyayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Katiba ile haijabadilika, kwa hiyo tunaitumia Katiba hii tulionyayo itupe nafasi tuandike hiyo Katiba mpya itakayokuja, kwa hiyo, Katiba hii ya sasa Rais yupo, vyombo vya dola vipo, tunachohitaji sasa ni kwamba tutumie nafasi hii tuandike hicho tunachokitaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo yapo malalamiko mengi yanasemma hata humu ndani ya Bunge tumesema kwanza yanahusu ardhi, tunasema Katiba ya sasa haijasema vizuri kuhusu ardhi, inasema Rais ndiyo mamiliki wa ardhi, watu wanasema hapana, hayo ni maoni mapya lakini ndani ya Katiba ya sasa yapo, lakini hatutaki hiyo tunataka nydingine mpya lakini ya leo tunaiheshimu hii iliyoko, yako malalamiko ya ardhi, yako malalamiko ya madini na rasilimali za nchi yetu na yako madaraka ya Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunahitaji pia na nafasi ya wanawake katika mustakabali wa nchi hii, siyo nafasi ya Viti Maalum, hapana, nafasi ya Kikatiba kuhusu nafasi ya wanawake, je hivi tunavyokwenda kwenye uchaguzi ndiyo itatupa nafasi sawa na wengine, wote hapa tunahitaji mabadiliko, lakini hatuwezi kuyadai leo tutayadai hapo wakati mchakato utakapokuwa tayari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nawaomba wanawake, wajitokeze katika hayo Mabaraza yatakayoundwa waende wakaseme tunataka nini kwa sababu nchi hii ni yetu, hata vijana nendeni, mimi nazungumzia wanawake, nasema twende huko hatutaki kitu cha kubandikiziwa, wengi wanasema tumepependelewa, hatutaki kupendelewa, tuna haki sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sisi ndiyo mama tuliozaa Watanzania wote, kwa hiyo, tunahitaji kuona sehemu sawa kabisa ya maendeleo ya nchi hii, tunataka yaingie kwenye Katiba. Ardhi kama nilivyosema, madini, nafasi za wanawake, vijana na makundi maalum yote, kwa hiyo tuitumie nafasi hii kuyaweka hayo mapya. Vile vile, Muungano tunautaka uweje, lakini kusema Muungano haupo, huo ni ukichaa kidogo. (*Makofii*)

Muungano upo na mtu anayesema haupo ni kama alivyosema Mheshimiwa Wasira jana kwamba, mtu mzima anapomdanganya mtu mzima mwenzake kuna mambo mawili yanayomsibu ama kidogo akili zimechanganyikiwa ama inawezekana kwamba anafikiri wenzake wote ni wajinga. Sasa mtu achague anataka nini katika kuwadanganya watu wazima. Tunachohitaji hapa si Katiba, tunachofanya hapa ni mchakato utakaotufikisha huko kwenye Katiba mpya, ndiyo tunachokifanya hatutungi Katiba mpya, Katiba bado ipo na tutifuata na ni lazima tuitii na ni lazima Katiba ya sasa ifanye kazi mpaka hapo tutakapotangaza Katiba mpya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna watu hapa tulipokuwa tunafanya uchaguzi mwaka jana walisema hivi wao wakishinda, nafikiri CHADEMA, baada ya siku mia moja watakuja na Katiba mpya, ndiyo kusema walipokuwa wanachewenda kwenye uchaguzi walikuwa na Katiba mfukoni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Rais Kikwete anasema mimi sitaki kuitoa ya kwangu, nataka Watanzania wote washiriki wake kwa waume kuandika Katiba mpya, sasa nani mwenye mawazo sahihi kwa wananchi Watanzania, yule aliyekuwa na Katiba yake mfukoni baada ya siku mia moja au sisi huku tunaosema huu mchakato utakuwa ni mrefu ili kila watu wafikiwe. Sasa mtu anasema tunatunga hapa Katiba, nafikiri baada ya Muswada huu kuitishwa na nawaomba tuunge mkono upite. Wajue kabisa wanachosema kwamba tunatunga Katiba hapa ni uwongo tena uliokithiri, tunachohitaji hapa ni kuweka taratibu zitakazotusaidia kufikia huko kwenye azma ya kuwa na Katiba mpya ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ili sasa tufikie hapo, lazima tuwe na sheria hii tutakayoipitisha kuhakikisha kwamba tutakuwa na jopo la watu yaani Tume, watu wangapi mimi sijui, najua sitakuwepo humo, lakini nitakuwa mmojawapo katika kutoa maoni yangu itakapofika wakati huo. Kila mtu hapa ana mawazo yake na kuacha kutoa mawazo ni uwoga, kwamba yale mnayowadanganya watu huko nje, wakisikia hapa unaunga mkono utaonekana kwamba kumbe mnawadanganya, kwa hiyo, mnaendeleza kuwadanganya wananchi kwamba huku ndani ya Bunge watu wanashughulikia habari za kutunga Katiba mpya. Hatujatunga Katiba mpya hapa na wala si kazi yetu kutunga Katiba mpya, hayo yako kwenye taratibu zitakazoletwa na Muswada huu, sisi kazi yetu kubwa hapa ni kuhakikisha kwamba taratibu hizo zinawekwa kisheria kwa kuwa sisi ndiyo wenye mamlaka na madaraka ya kisheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa tunavyo vyombo vingi, vingine vinaitwa vya wananchi, vingine vinaitwa sijui vya vitu gani na majukwaa mbalimbali, tunavyo vyombo vipyta, wana uhuru wa kusema wanachokitaka lakini wajue kabisa mamlaka ya kutunga sheria ya nchi hii yako kwenye Bunge hili, wao hawatapata nafasi hata siku moja ya kutunga sheria mpaka waje waingie ndani ya Bunge hili, aapishwe ndani ya Bunge, ndipo anaweza kuja kutunga sheria. Ndiyo maana wanaharakati hao wengine wameingia ndani ya Bunge kwa ajili ya uanaharakati wao, wanadhani hapa ni mahali pa harakati, hapana hapa ni mahali pa kutunga sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kama mtu ana wazo lake, msikilize anachosema, kama hilitaki wewe wazo lake na wewe simama ujibu, lakini kwa kuwa mtu anasema usilotlaka kuliskia, unatoka nje, huo ni woga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia niseme kwamba, si kweli kwamba hawakutoa maoni yao, wametoa mbona msemaji wao mkuu amesema, si tumemsikiliza humu ndani, si yamo kwenye *Hansard*, sasa wanatoka kufanya nini kwa sababu wanajua kwamba watashindwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema tuisifikishe nchi yetu hapo na nawaomba Watanzania waelewe kwamba, kuna watu hapa kazi yao wanataka la kwao ndiyo liheshimike na lisikilizwe, msipowasilikiza wewe siyo sahihi na wamejiwekea vikundi vya wananchi na wao kuwa wasemaji wa wananchi, hivyo navyo nasema tufike mahali ambapo tunaukataa, tunaukataa kabisa kabisa mtindo huo, kila mtu hapa amezaliwa na ana haki ya kusikilizwa na ndiyo Katiba yetu inavyosema na mtu atoe maoni yake kwa uhuru na mahali pa kutolea maneno hayo bila hata mtu kuulizwa kwa nini umesema, ni hapa ndani ya Bunge, hapa ndani ya Bunge unaweza tu kusema ila yathibitishe hayo unayoyasema...

SPIKA: Ahsante.

MHE. ANNA MARGARETH ABDALLAH: Ndiyo peke yake.

SPIKA: Ahsante.

MHE. ANNA MARGARETH ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Spika, na mimi nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kusema machache yale ambayo ninayo. Lakini nichukue nafasi hii pia kumpongeza Waziri, nipongeze na Kamati pia, Mwanasheria, ambao kwa kweli kazi kubwa wameifanya kutuletea vipengele 34 ambayo ukiviangalia wamevijadili na wamevipima na wameangalia wanaona kwamba ni vipengele muhimu sana kuelekea katika kutengeneza Katiba mpya au Katiba ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna Miswada mingi sana ambayo tumepitisha hapa, kwa mfano juzi tulikuwa na Muswada wa Sheria ya Ununuzi na ulikuwa mzuri sana na ndugu zetu kwa kweli walitoa mchango mzuri, walichangia vizuri sana. Nakumbuka sana ndugu yetu Mheshimiwa Mnyika, alisema vizuri sana Mheshimiwa Zambi alisema vizuri, Mheshimiwa Mpina. Wote walisema vizuri wakachangia wakarekebisha pale ambapo palikuwa hapako sahihi. Nafikiri kwamba kwa kuleta Muswada huu ndugu zetu wangetusaidia kutengeneza kitu ambacho ni kizuri pengine

tungeanza kukosoana humu ndani, lakini kukimbia kwa kweli kumetutisha. Ni jana au juzi nilikutana na watu wengi, wengine wametoka kwangu katika Jimbo langu la Mbeya, wengine wametoka Mbeya Mjini na wanasema wametoka huko wameletwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba huu Muswada haupiti.

Mheshimiwa Spika, baadaye nilipokuwa naongea nao wakasema bwana, tulipokaa tukashangaa watu wa kutoka Zanzibar na kutoka kila mahali katika nchi walikuwa hapa wanazungumza, lakini tukagundua kumbe walio wengi waliokuja ni watu wa CHADEMA, lakini tulipoongea nao wakasema, bwana baada ya kuona kwamba wamechangia watu wengi tukaona kwamba hakukuwa na sababu ya sisi kuja hapa. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Ni kweli.

MHE. LUCKSON N. MWANJALE: Wakasema tuliiitia tu na kupewa nauli ya kuja hapa na kulala, lakini wakasema kumbe Muswada huu ni mzuri. Nikasema jamani huu Muswada mdogo sana, ni Muswada ambao unaiwezesha ile Tume kuja kwenu huko na kama kutakuwa na mapungufu, basi huko ndiko mtakaa muweze kukosoa yale ambayo ni mapungufu. Lakini ukweli hata ndugu zetu wakikimbia bado kuna watu wazuri sana CHADEMA ambao wanajua kukosoa, ni wasomi wazuri, wanajua sheria, wangetusaidia sana kuhakikisha kwamba huu Muswada ambao tunautengeneza utatusaidia, lakini sasa wamekimbia. Maana yake nini, kwa hiyo, ndugu zangu Wabunge tuelewe wazi kwamba, kumbe kulikuwa na watu ambao wameshinkizwa kuja hapa kuangalia na kuweka mgomo ili Muswada huu usiweze kujadiliwa tena. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niseme wazi, nikamwambia huyo mtu kama huu Muswada ni Serikali imeleta kwa hila basi CHADEMA mtasimama, lakini kama umeletwa kwa nia nzuri kwamba Watanzania wajadili, Watanzania waweze kuja hatima ya Katiba yao ambayo wanaitaka na wamelalamika mara nyingi, basi suala hili la Katiba litaendeleaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikaweka maneno ya laana lakini siyo laana maana hata kwenye Biblia inasema hivyo hivyo. Kuna mtu mmoja alisema kuwa, kama mtu huyu ambaye amesimama kuhubiri amesema maneno haya kutoka kwa Mungu, basi mambo yake yatasimama, lakini kama hajaletwa na Mungu mambo yake hayatasimama. Sisi tunasema huu Muswada tuna hakika kwamba, kwa kweli umeletwa kwa nia nzuri. Lakini nafikiri kuna nia ya makusudi ya kusababisha Muswada huu usiweze kuchangiwa na wananchi kwa sababu wanataka kutumia njia ya *ku-delay* Muswada huu, *uki-delay* Muswada huu ukaja baadaye na baadaye tunaingia kwenye uchaguzi, maana yake tunapoingia kwenye uchaguzi tutakuwa na *pressure* ya Muswada wenyewe, halafu tunakuwa na *pressure* ya uchaguzi kwa maana hiyo ni kwamba, watajipatia sifa kubwa sana ya kuhakikisha kwamba wao wanashinda kwa sababu mtakuwa mnahangaika na uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, naomba na naunga mkono kwa asilimia mia moja ili Muswada huu upite na ili wananchi popote walipo wakatoe mawazo yao na Katiba hiyo mpya inayodaiwa basi ikafanyike. Kuna nchi zina Katiba miaka mingi na hawaigusi, ni mambo madogo madogo tu wanaweka, sasa kama kila wakati tutakuwa na watu wa namna hii na NGOs ambazo zimeundwa, kazi yao kubwa ni kukosoa Serikali, sawa kukosoa hatukatai maana ni lazima ukosolewe. Lakini huwezi ukakosoa kwa msingi huo hata kama wanahitaji mabadiliko yafanyike lakini mabadiliko yafanyike kwa utaratibu siyo kwa njia hiyo na ukigoma na kuzila na roho ya kuzila mara nyingi siyo roho nzuri, kwa sababu ukizila maana yake ni kwamba umeshindwa huna njia nyingine tena ya kufanya na ndiyo maana watu wengine wamejua kwa sababu wamezila, wanaona hakuna maana yoyote ya kuishi anaamua kujiu. Sasa ni kwa nini tuzile kwa kutengeneza kitu kama hiki ambacho ni kizuri?

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni sahihi kwani nilikuwa najaribu kupidia *argument* yao kubwa kwa kweli ni kwamba Muswada huu uwe *delayed*. Lakini tuliiitia Dar es Salaam, tuliiitia Dodoma na waliitwa watu Zanzibar, wakajadili na kulikuwa na maelfu na mamia ya watu kwenye Muswada huo, waliujadili wamezungumza kwa uhakika maana hata ungepeleka huko vijiji ni kwani wote watajadili? Hivi utapeleka Mbeya Vijiji watu wote 200,000 watakuja wajadili Muswada? Haitawezekana! Lakini kutakuwa na watu ambao pengine hata wakija mia moja au mia mbili

mtapewa nafasi wote mseme? Hata Bunge hili Wabunge tupo zaidi ya mia tatu, hivi wote tutasimama na kuzungumza? Pengine Wabunge wachache watapata nafasi kuzungumza. Ndugu yangu Shah amesema kwamba ni Wabunge 50 tu wamechangia mpaka sasa Muswada na utakwisha kesho au kesho kutwa, hivi tutazungumza wote? Hata huko utakakokwenda tungepeleka huko wasingweza kuchangia watu wote, ni wachache tu watakaochangia. (Makof)

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni mzuri na utakuja kwenu, mtatoa maoni na kama mtaona kwamba kuwa na mambo ambayo hayaendi sawasawa si mtasema? Kwa nini basi muanze kuzuia hapa? Maana yake mna mbinu ya kutaka kuchelewesha Muswada usiweze kujadiliwa na wananchi wasitoe maoni yao na hatimaye ili mtupe *pressure* wakati tunakwenda kwenye uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa ujumla naunga mkono hoja hii hata kama kutakuwa na mtu mmoja atakataa, lakini ukweli ni kwamba, hakuna kitu ambacho ni kipyä katika Muswada huu kwani kila kitu kipo sahihi kabisa na Wabunge wamejadili Muswada kwa uhakika na kila kitu kimejadiliwa kwani hakuna kitu kilichofichwa. Kwa hiyo, kusema sijui tupeleke kwa wananchi haitakuwa na maana yoyote kwani wananchi wametuchagua na tumekuja Bungeni kwa kura na kila mmoja amekuja hapa kwa kura, tunazungumza kwa niaba ya wananchi kwa sababu kuna mambo ambayo wananchi tunawazungumzia Bungeni, si wote wanaoweza kuja kudai maji hapa, si wote watakuja hapa kudai umeme, lakini kwa niaba yao tunazungumza sisi. Sasa kwa nini leo hii tuwaambie kwamba hatutaki, mbona Miswada mingine hawajawahi kuikataa, kwa nini Muswada huu waukatae? (Makof)

Mheshimiwa Spika, juzi tumepitisha Muswada wa Ununuzi, wote tuluijadili na kwa kweli mengi yalisahihishwa, sasa huu ni kwa nini wasiukubali? Kwa hiyo, naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja na naomba kwa niaba ya wananchi wangu wa Mbeya Vijiji kuunga mkono Muswada huu upite.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (Makof)

MWENYEKITI: Ahsante Mchungaji na sasa namwita Mheshimiwa Jaddy Jaddy atafuatiwa na Mheshimiwa Herbert J. Mntangi na Mheshimiwa Rweikiza ajiandae.

MHE. JADDY SIMAI JADDY: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia machache katika Muswada ulio mbele yetu. Yangu ni machache sana katika Muswada huu kwa sababu, kwanza, na-*declare interest* kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

SPIKA: Tunamsikia vizuri? Ungehama *microphone* tafadhal!

MHE. JADDY SIMAI JADDY: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Natumaini nasikika sasa.

Mheshimiwa Spika, Muswada ulio mbele yetu umekuja wakati muafaka na wakati ambao Tanzania tulikuwa tunaelekea sehemu mbaya sana ya kufarakana kati ya Tanganyika kwa maana ya Tanzania Bara na Visiwani na ni chimbuko letu sisi wenyewe kwa kutaka Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, nachukua mchakato ambao tunakwenda nao sasa hivi, samahani sana, lakini ni sawa na Mama Mjamzito kwamba tumechukua ujauzito sasa na hatuna budi kuuchungachunga kiasi kwamba kilichopo tumboni kitoke salama. (Makof)

Mheshimiwa Spika, napatwa na mshangao mkubwa sana na ndugu zetu wa CHADEMA, dhana ya kwamba Mheshimiwa Rais amepewa Mamlaka makubwa sana katika Sheria hii hainilingii akilini kwa kweli kwa sababu kwangu suala la kuteua wajumbe wa Kamati nalionia kama ni dogo mno kuliko suala la kumpa Mamlaka Rais ya kutia saini, kwamba awe ndiyo mwamuzi wa mwisho. Sasa nikichukua suala la uteuzi wa Wajumbe wa Kamati na suala la hiari ya kutia saini na kutokutia saini mwisho wa mchakato tuliokwenda nao Bungeni sasa hivi, naona Mamlaka kubwa zaidi ni ya utiaji wa saini. Rais anaweza akasema hatii saini Sheria hii, nani atakamata rungu

amwambie tia saini Sheria hii? Kwa maana hiyo hiari anayo Mheshimiwa Rais, kwa hiyo, nadhani ni hatua moja kubwa sana ambayo CHADEMA ilikuwa kama kweli wana nia safi ya kusema sasa sisi tunapinda kuwepo kwa Muswada huo unaokuja katika Bunge hili kupelekewa Mheshimiwa Rais kutia saini, badala ya kusema kwamba amepewa Mamlaka makubwa ya kuteua Wajumbe wa Kamati ile.

Mheshimiwa Spika, Bunge hili linafanya kazi kubwa sana, sasa hivi Wabunge wapo katika kuelimisha jamii kwamba nini kinaendelea ndani ya Bunge. Inawezekana kwa wananchi wanachukuliwa bila kuelewa wapi wanakwenda na wanachukuliwa kiasi kwamba hawaelewi nini wanakifanya.

Mheshimiwa Spika, Warusi walikuwa na maisha fulani ya maajabu sana ya kila kitu kukaa foleni, unawenza kumkuta Mrusi amekaa kwenye foleni hatambui kinachotaka kuuzwa ni kitu gani yeze amekaa tu kwenye foleni. Muulize kuna nini kinataka kuuzwa huko mbele, atakwambia sijui ni nini. Sasa yawezekana na wananchi wetu wanachukuliwa katika hali hii na hao ambao wanajiita wanaharakati bila kuelewa ni nini ambacho kinaendelea.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamesimama katika Bunge hili na kueleza kitu ambacho tunaendelea kukijadili katika Bunge letu Tukufu. Pia napenda kuwaomba wananchi kwamba waelewe ni nini ambacho Wabunge tulipo katika Bunge hili tunakijadili. Hatujadili Katiba bali tunajadili Sheria ya kuanzisha mchakato wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, Wanaharakati mawazo walijonayo ni ya CHADEMA, kwa mara ya kwanza hawa ambao wanajiita Jukwaa la Katiba walikuja mbele ya Kamati ya Katiba na Sheria, utangulizi wao wote ulikuwa na mawazo yote ya ki-CHADEMA kwamba ooh! Maana yake unajua hii ndio mara ya kwanza na kadhalika yaani ni mambo ya ajabu ajabu tu. Kwa hiyo, tulitambua kabisa kwamba uwepo wao katika Kamati ya Katiba ni maelekezo kutoka katika chama cha CHADEMA, kwa hiyo, hatuwashangai. Lakini ilitupa mshangao kwani hata baadhi ya wasomi waliofika mbele ya Kamati yetu walikuja na mawazo ya maajabu sana pamoja na kwamba walikuwa ni wasomi wallobobe, tuliwashangaa sana. Hii ni hatari sana.

Mheshimiwa Spika, napata faraja kwamba nitakuwa ni miongoni mwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa kuizaa Tanzania mpya. Lakini nitasikitika sana kwa kuwa nitakuwa ni miongoni mwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wanaokwenda kuiua Tanzania. Kama hatukuwa na hadhari ya mchakato ambao tunaendelea nao tunachokitafuta hatutakipata na matokeo yake tutaparaganyika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kutoa hadhari kwa wananchi, twende na mchakato tupate kile ambacho siku nyngi tulikuwa tukikitafuta. Tulichokuwa tunakitafuta siku nyngi ni Katiba ambayo itakuwa imeridhiwa na wananchi kwa ujumla wao badala ya ile iliyopo sasa hivi ambayo inaambiwa kwamba ilipitishwa kwa utashi tu wa Marais wawili wa mwanzo wa Jamhuri ya watu wa Zanzibar na Jamhuri ya watu wa Tanganyika. Tukiipata hii sasa hakutakuwa na hata mmoja wa kumwelekezea kidole mwenzake kwamba wewe ndio uliyataka haya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba wananchi tustahimili na watuelewe kwamba tupo katika harakati za kutafuta Katiba mpya ya Tanzania ambayo itatufanya tuwe wamoja, itatufanya tuweze kuaminiana badala ya kuchukiana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika Muswada huu mahususi. Lakini pia ni lazima niseme kwamba, nimekaa kimya kwa muda kidogo ili kuwasikiliza Waheshimiwa Wabunge na dhamira yangu kubwa ilikuwa ni kutazama upeo na uwezo wa Waheshimiwa Wabunge ambao wameingia Bungeni kwa mara ya kwanza. Naomba nikiri kwamba, nina hakika ufahamu na uelewa wao ni mkubwa sana na kwa hakika vijana waliopo na wanaozungumza wanazungumza

kwa hekima na kwa busara. Nina uhakika watasaidia sana kuweka mwelekeo mzuri kwa kizazi kijacho. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Katiba iliyopo ni Katiba ambayo sisi tumeshiriki kuitengeneza, tunahitaji Katiba mpya kwa sababu ya mabadiliko ya kidunia kwa maandalizi ya kizazi kijacho na nafurahi kwamba vijana wamepata nafasi ya kuingia katika Bunge hili na maandalizi watafanya wao ya kuhakikisha kizazi kijacho kinapata Katiba njema.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na tutazame wenzetu wamefanya nini. Kanuni za Bunge ni Kanuni ambazo lazima zihestimiwe, hakuna sababu ya kwenda kinyume cha Kanuni za Bunge, kwa hiyo, utaratibu tunaoufanya ni sehemu ya Kanuni za Bunge na tunatekeleza hivyo. Wenzetu wametoa michango yao, lakini naomba nitoe mfano mdogo sana.

Ukitazama kitabu cha maoni na ushauri wa Kamati ya Katiba kinazungumzia Muswada wa Sheria ambaa umejadiliwa na Kamati ambayo ni halali, Kamati hiyo ina watu 22 na nataka niwahakikishieni kwamba mionganoni mwa hao watu watu 22 wapo Wanachama wa CHADEMA, wapo na wanajijua. Kwa hiyo, wapo jumla kama 11 ni karibu 48%, wamekaa na wametoa taarifa ya Kamati na wote majina yao yametajwa wakati Mwenyekiti anatoa taarifa, maana yake wameshiriki na kwa hakika nawapongeza kwa sababu Kamati ile imetoa mapendekezo mengi sana ya busara na mengi yamekubaliwa na ukitazama mchakato ule wa mabadiliko Mheshimiwa Waziri ameyapokea maana yake pia amepokea mapendekezo yao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ukitazama na kuisoma kwa makini taarifa alioitoa Mheshimiwa Tundu Lissu, ndiyo utajua kwamba taarifa hii ni ya kwake, kichwa cha habari kinasema; Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani siyo maoni ya Kambi ya Upinzani, siyo maoni ya Upinzani ni ya kwake Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani na hili limethibitishwa baadhi ya viongozi wengine wa upinzani waliopo hapa ndani wamesema kwamba si maoni yao. Sasa kama hivyo ndivyo tafsiri yake nyingine ni nini? Wenzetu wa CHADEMA wapo 48 nadhani, lakini taarifa hii ni ya kwake yeze peke yake, kwa hiyo Wabunge 47 maoni yao hayapo. Nini kilichotokea? Kwa sababu yeze maoni yake ameshayatoa sasa ameshawishi wenzake 47 wasipate nafasi ya kutoa maoni yao ndani ya Bunge hili. Sisi wengine tunatoa maoni yetu lakini wale wenzake 47 amewashawishi wametoka hawatoi maoni yao, jambo baya sana hili, ni ubinafsi wa hali ya juu huo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niseme ukweli kwamba, wote tunakaa na kuzungumza nao na kucheka nao kila siku lakini siyo wote 47 ambaa wametaka kudhamiria kutoka ndani ya Bunge, wametoka kwa agizo la uongozi wa chama chao, ndicho kilichowafanya watoke. Kwa hiyo, chama chao pia kimewanyima haki Wanachama wake kutoa maoni yao ndani ya Bunge. Huu siyo uongozi mzuri kwa sababu pamoja na kwamba hao ni Wanachama, nao pia wamechaguliwa kwa kura za umma, wanawawakilisha wananchi wa Tanzania kwa nini muwanyime haki? Wanatoka kwa sababu ya woga kwamba asipotoka ataitwa kwenye chama kwenda kuhojija, lakini wengi wanaskitika hawakupata nafasi ya kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Spika, lakini tutazame maoni ya mwenzetu huyu mmoja. Katika Muswada amechangia na kutoa maoni kwenye zaidi ya vifungu 40, naweza nikavitaja vyote lakini naomba nitaje vichache tu kwa sababu ya muda.

Kifungu cha 6(1) na (3), kifungu cha 7(2), kifungu cha 13(1) na (2), kifungu cha 8(1), (2) na (3) vyote hivyo ametoa maoni yake. Lakini kikubwa ambacho leo nataka kukizungumzia kwenye baadhi ya maoni yake ni ile kauli ya Urais wa Kifalme, kwamba utawala uliopo sasa na hao waliopita ni utawala wa Kifalme. Sasa tuangalie utawala wa kifalme ukoje halafu tulinganishe kama kweli hizi awamu zetu zote nne zilikuwa ni tawala za kifalme.

Mheshimiwa Spika, kwanza, utawala wa kifalme hawachaguliwi kwa kupigiwa kura na wananchi wote wa nchi nzima, hiyo ni moja na nitataja chache. Lakini wafalme huwa wanatawala kwa ukoo tena kwa kurithishana. (*Makofî*)

Jambo la tatu, Wafalme hutawala hadi kufa kwao, wakishakufa anayefuatia ni mrithi wa ukoo kutoka katika familia yao. Jambo lingine ukitazama viongozi hawa wa kifalme wanaabudiwa, watu huwapigia magoti wanalo sema wao ndiyo la mwisho. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa hebu tutazame haya machache niliyosema, hivi kweli katika awamu hizi nne haya yalikuwa kweli yanafanyika? Hapana! Baba wa Taifa, alitokea katika familia hizo za kichifu lakini alipokuwa anataka kuwa Rais wa nchi hii, alipewa ridhaa na wananchi wa Tanganyika wote na siyo wale wa kule Musoma peke yao. Kwa hiyo, hilo halikuwepo na hizo awamu nydingine zote zilizofuatia dalili hizo hazipo.

Mheshimiwa Spika, jambo moja ambalo tunapaswa kuliangalia pia, tunatoa maoni, hatutungi Katiba. Leo nina furaha kwamba, tumepata nafasi ya kuwaona ndani ya Bunge hili wasomi wengi wa vyuo mbalimbali waliopata nafasi kuingia hapa. Nina uhakika safari hii wanashuhudia kwamba, tunachofanya ni kutengeneza Muswada, siwezi nikaenda kukusanya maoni ya Katiba Mpya bila kuwa na mpango maalum unaonilinda mimi au taasisi nydingine yoyote. Hakuna kitu kinachokulinda wewe na kukupa hadhi ya kufanya haya unayotakiwa kuyafanya isipokuwa sheria. Sasa sheria ndiyo hii tunayoitunga. Tuifanyie marekebisho tuiboreshe ili tutakapoanza kazi ile basi tutakuwa tunafanya kazi za uhakika.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, makundi maalum kutakuwa na wajumbe mia moja kumi na sita (116). Hii ni hesabu ambayo tumeiweka katika Muswada lakini isiwe kwamba, ndiyo haiwezekani kuongezwa wala kupunguzwa. Sioni sababu yoyote ya kuipunguza, busara zangu zinanituma uwezekano wa kuongeza idadi hiyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ukisema una kundi la wakulima, wakulima tunatofautiana katika nchi hii. Wako wa karafuu, korosho, pamba, wako wa machungwa kule Muheza na kadhalika. Sasa utawashirikishaje wote? Wana chama kimoja cha wakulima wote Tanzania nzima?

MBUNGE FULANI: Hapana!

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Hapana! Kwa hiyo, lazima uwapange kwa makundi ili ujue wanawakilishwa kikamilifu. Kwa hiyo, ukisema utakuwa na mmoja, nasema siyo busara kuwa na mmoja. Tuwe na wengi zaidi ili wakulima wa mazao mbalimbali waweze kuwakilishwa vizuri.

Nenda pia katika maeneo mengine hata ya akinamama, hata ya wale mavu, nafasi hizo lazima zlongezeko. Lakini kikubwa kinachofanyika ni nini? Watu wanadhani kwamba, Rais ndiye atakayepewa mamlaka ya kuwateua watu wote hao. Muswada unaweza ukasema hivyo, lakini hapanal! Wakulima watatoa mapendekezo ya mwakilishi wao, wao wenywewe na hatimaye Rais ataridhia. Naomba neno hili la kuridhia liingizwe katika Muswada wetu. Badala ya kusema Rais atateua watu wanadhani Rais ndiye atakayeteua kila kitu na kila mahali, lakini uwakilishi huu wa makundi maalum, makundi yenewe yatatoa mapendekezo ya wawakilishi wao na Rais ataridhia.

Mheshimiwa Spika, naomba hizi nafasi za uwakilishi ziongezwe, *tusiji-limit* kwenye mia moja na kumi na sita (116), makundi ni mengi na yote yanahitaji haki sawa na kuhudumiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, muda wangu umekwisha. Naomba nirudie kuwapongeza wale wote waliochangia kwa busara na kwa heshima. Siku zote Katiba inatoka katika moyo lakini lazima ichangiwe kwa hekima na busara. Waliopo ndani hapa wanaotoa michango yao wana hekima na busara. Mwenyezi Mungu atawabariki wote na nina uhakika Katiba Mpya itapatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof!*)

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ili nami nichangie katika Muswada huu muhimu. Kabla ya yote ni sema kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, kwa hiyo, nimeshiriki kikamilifu katika mchakato mzima hadi hapa tulipofikia.

Mheshimiwa Spika, mbele yetu tuna Muswada mzuri kabisa unaolenga kutusaidia tuweze kufikia hatua ya kutunga Katiba yetu nyingine. Ni mzuri na kwa hiyo, naunga mkono Muswada huu. (*Makofî*)

Muswada huu ni wa maandalizi ya mchakato wa Katiba Mpya. Una mambo mbalimbali, mambo ya kuunda Tume, jinsi ambavyo Tume itafanya kazi, Bunge Maalum au Bunge la Katiba, Kura za maoni za wananchi wote na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nipayendekeze moja kwa moja kwamba, katika Muswada huu nina mambo mawili ambayo nayapendekeza yabadilishwe. Jambo la kwanza ni jina fupi (*short title*). Jina fupi la Muswada huu kwenye lile toleo la Kiswahili linasomeka: "Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011" na kwenye toleo la Ingereza: "*The Constitutional Review Act, 2011*."

Mheshimiwa Spika, nipayendekeza kwamba, katika toleo la Kiswahili isomeke ifuatavyo: "Sheria ya Kutunga Katiba Mpya ya 2011" na Ingereza isomeke: "*An Act for The Making of A New Constitution 2011*." Sababu ni nini? Ni kwamba, unaposema *Constitutional Review Act* kwa Wanasheria review ina maana ambayo wanafahamu ni kurudia. Kwa mfano, kama ni hukumu unamwomba Hakimu yule aliyetoe hukumu arudie hukumu yake upya, ahukumu upya. Kwa English ya kawaada review ina maana ya kurudia au mapitio.

Mheshimiwa Spika, kwenye Kiswahili mabadiliko hayaleti maana halisi ya kitu kipyaa, yanaleta maana ya kwamba, unabadi hapa au pale, unarekebisha hapa au pale, kifungu kimoja au viwili au vitatu, haina maana halisi ya kutunga Katiba Mpya. Ndiyo maana hawa wanaotaka kupotosha wanatumia maneno haya kupotosha wananchi kwamba, sheria inayoshughulikiwa sasa hivi ni ya kuchakachua Katiba kwa maslahi ya Serikali au CCM, jambo ambalo si kweli. Kwa hiyo, kuondoa utata huu tuwe na maneno ambayo ni moja kwa moja kwamba, tunatunga Katiba Mpya. Tuseme, Sheria ya Kutunga Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la pili ni kuhusu uwepo wa Bunge Maalum au Bunge la Katiba, kifungu cha 20 hadi 26. Mawazo yangu ni kwamba, tusiwe na Bunge la Katiba, tuwe na Tume ipite kwa wananchi ichukue maoni, ichambue maoni, itengeneze Rasimu ya Katiba, iende kwa wananchi moja kwa moja. Turuke ngazi ya Bunge kwa sababu demokrasia tuliyonayo dunia nzima ni ya aina mbili; ama ya moja kwa moja, ama ya uwakilishi.

Mheshimiwa Spika, uwakilishi ni kama hapa katika Bunge hili. Tunatunga sheria kwa niaba ya wananchi. Tunazungumza bajeti na mambo mengine kwa niaba ya wananchi. Hawaingii kutunga sheria wenyewe au hawapitishi bajeti wenyewe, ni kwa uwakilishi.

Mheshimiwa Spika, demokrasi nyingine ni ya moja kwa moja. Wananchi wenyewe wanafanya jambo lao wao wenyewe, kama uchaguzi mkuu wa Rais na Wabunge, wanapiga kura wenyewe hawakilishi. Sasa ukiwa na Bunge la Katiba ina maana kwamba, wamewakilishi kwenye kuitisha Katiba. Halafu tena uwe na Kura ya Maoni, wamepiga kura wenyewe. Unakuwa na vitu viwili kwa wakati mmoja ambavyo siyo lazima. Unakuwa na uwakilishi kwa maana ya Bunge la Katiba na moja kwa moja kwa maana ya kupiga Kura ya Maoni. Nasema hii haina maana, haina ulazima. (*Makofî*)

Turuke moja. Dunia nzima wanaofanya kazi kama hii ya kubadilisha Katiba wanachukua moja wapo, ama Bunge la Katiba ama Kura ya Maoni 'referendum' hawawi na mbili. Kati ya nchi mia moja zinazofanya hivi nchi tisini na saba zinakuwa na hatua mojawapo, tatu ndiyo zinakuwa na hatua zote mbili. Sasa sioni kwa nini Tanzania iwe ni moja ya zile tatu katika mia moja, kuwa na hatua zote mbili yaani Bunge la Katiba na Kura ya Maoni. Hii ina mchakato mrefu zaidi, itasumbua sana kisiasa na kimchakato, ina gharama kubwa, turuke ile ya Bunge la Katiba twende moja kwa moja kwenye Kura ya Maoni.

Mheshimiwa Spika, nikirudi kwa wenzetu ambaa wanapotosha wananchi na kusema maneno ambayo siyo ya kweli na kuvuruga hali ya hewa, niseme kwamba hawa wana ajenda yao binafsi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Tumekaa kwenye Kamati hiyo muda mrefu, tumezungumza mambo ya Muswada huu na wenyewe wameshiriki. Tangu kule imekuwa ni vurugu karibu ngumi zipigwe. Ukichangia jambo ambalo hawalipendi wanasisimama, wanaleta vurugu, wanataka mawazo yao ndiyo peke yake yasikilizwe. Nikajiliza; hawa wana lengo gan? Huko nyuma ndiyo walikuwa mstari wa mbele kusukuma tuwe na Katiba mpya, tuwe na Katiba Mpya haraka haraka. Kwenye llani yao ya CHADEMA wanasema ndani ya siku mia moja baada ya kutwaa madaraka ya Serikali, watakuja na Katiba Mpya. Sasa leo ndiyo wamegeuka hawataki Katiba tena. Sasa tunajiiliza kwa nini? Sababu ziko wazi.

Mheshimiwa Spika, kipindi kile kabla ya uchaguzi walitaka Katiba Mpya ifanyike haraka haraka, ivrugwe vurugwe, ivurundwe vurundwe, wafanye mambo yao wayaingize mle ndani bila utaratibu wa kutosha, bila tathmini ya kutosha ili waone kama wataingiza lkulu kwa njia za mkato.

Mheshimiwa Spika, nia yao haikutimia. Sasa wakaona Serikali imechukua jambo hili imeazimia kwamba, Katiba Mpya itengenezwe, wakaona waikwamishe ili Serikali ioneckane haiwezi, imeshindwa, ili baadaye kabla ya uchaguzi ujao wa 2015 huko waanze tena kelele. Wapige kelele Katiba Mpya, Katiba Mpya! Ifanyike haraka haraka, waingize mambo yao ambayo siyo sahihi, waone kama yatawaingiza kwenye nafasi ambazo wanazitaka. Sasa nasema tusikubali tuendelee na kazi hii ya kutunga Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, malalamiko yao yote wanayoyasema Rais ana mamlaka makubwa, nasema Rais madaraka hayo hakujipa mwenyewe, kapewa na Katiba iliyopo. Kama wana matatizo na hilo waje humu ndani tushirikiane, wachangie waondoe vifungu vile. Mahali pa kuondoa vifungu hivyo ni hapa siyo huko nje walipo, ni humu ndani. Wasikae nje, waje humu ndani washiriki, wachangie, tuondoe yale mambo ambayo yanawakera kama wataweza kutushawishi sisi wote tukubaliane nao, basi tupitishe mawazo yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia kusimama hapa leo. Lakini la pili, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuweza kuchangia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, mara tu baada ya uchaguzi wa 2010 wa mwezi wa Oktoba, Wabunge ambao tumo humu ndani pamoja na Wabunge ambao wametoka, tulikuwa tunaitwa Wabunge Wateule na Ubunge wetu ulikamilika pale tulipokula kiapo cha utiifu. Katika kiapo hicho nakumbuka yamo maneno yanayosema kuwa; ‘Nitaitetea na kuilinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.’ Haidhuru Katiba yenyewe pengine ina mapungufu na ndiyo maana kuna nia ya kujenga Katiba Mpya, lakini inaonekana wenzetu wakati wanataka kukamilisha Ubunge wao Katiba ile waliikubali. Leo katika mchakato wa kupata Katiba Mpya, Katiba ile wameikataa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, unaposema utaitii na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katiba ina sehemu nyingi, lakini nichukue sehemu moja tu ambayo inazungumzia uwepo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuanzia Ibara ya 102 mpaka Ibara ya 107. Katika Ibara hizo unakuta uwepo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, uwepo wa Baraza la Mapinduzi na uwepo wa Baraza la Wawakilishi. Sasa leo unapokaa Bungeni ukaikejeli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ukawaona Wazanzibari hawana haki, ukumbuke kuwa umekula kiapo. Je, tukuhesabu hapa kiapo chako ni vipi? (*Makof*)

Kubali mapungufu yaliyomo katika Katiba lakini bado uwepo hapa katika kujadili ili hizo dosari zinazoonekana basi ziondoshwe. Kwa hiyo, wenzetu ilipaswa kwa kweli kwa vyovyote, kwa busara za kawaida tu wabakie humu ili tuendelee na mchakato huu.

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, alidhihirisha kuwa Zanzibar ni kama inapendelewa katika hotuba yake. Kwa kweli, nimeuangalia Muswada huu nimeshindwa

kuona wapi ambapo tumependelewa. Ukiangalia utaratibu wa kupiga kura katika Bunge la Kutunga Katiba, ni lazima zipatikane theluthi mbili za Wazanzibari na theluthi mbili za Watanzania Bara. (*Makofî*)

Sasa unaposema kuwemo kifungu hicho mfano, tumependelewa kwa Mwanasheria huyu kifungu hiki ilikuwa kiwekwe vipi? Labda alikuwa akitaka uchukuliwe ujumla wa kura za Watanzania kwa maana ya Wapiga kura laki tano na kidogo wa Zanzibar na milioni kumi na tisa Tanzania Bara, labda uchukuliwe ujumla wa matokeo haya.

Mheshimiwa Spika, lakini unapofanya hivyo maana yake unasema kuwa hii ni Serikali ya Muungano wa Serikali moja. Kwa hiyo, uwepo wa Serikali mbili ni lazima udhihirishwe kwa Zanzibar awe na maamuzi na Tanzania Bara awe na maamuzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine kama kupendelewa labda ni kuambiwa katika Kura ya Maoni ipatikane zaidi ya asilimia hamsini na moja (51%) ya Wazanzibari na asilimia hamsini na moja (51%) ya Watanzania Bara. Sasa unapochukua hilo ukalisema liwe pengine tusipendelee maana tupige kura kwa ujumla basi narudia kule kule ambapo nimekwishalieleza kwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Tume ambayo inasemwa kuwa na ndivyo ilivyo kuwa Wajumbe wawe sawa, nadhani hii Tume kwa kweli siyo Tume ya maamuzi, ni Tume ya kiutendaji. Kwa hiyo, unapochagua Wajumbe saba huku na Wajumbe saba huku, bado hujaleta athari katika maamuzi ya mchakato mzima. Kwa hiyo, suala la kuwa Zanzibar imependelewa kwa kweli sikuona mantiki yake, katika suala hili la Muswada huu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niwasihî wenzetu kwa kweli, maadamu wamekula kiapo cha kuitii na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, basi waone kuwa wamekosea na wawaombe radhi Watanzania na Wazanzibari kwa ujumla. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu niseme kuna sehemu katika kifungu namba 13(3) ambapo hapa anakuwepo Katibu wa Tume. Pale imesema kuwa, Katibu huyu lazima awe Mtumishi wa Serikali. Napendekeza kuwa hapa pasiwe na ulazima huo, bali apatikane mtu mwenye sifa ambaye amestaafu. Wako Majaji wazuri tu wamestaafu na bado wana uwezo waweze kulishughulikia suala hili.

Mheshimiwa Spika, lingine katika Muswada huu kuna Tume na Bunge Maalum la Katiba na Bunge hili na Tume hii litafanya matumizi makubwa kwa kweli kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, lakini hakuna kifungu ambacho kinasema Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali atakagua hesabu hizi. Kwa hiyo, nashauri kuwepo kifungu ambacho Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mara tu Tume itakapokamilisha kazi zake na Bunge la Katiba litakapokamilisha utaratibu wake basi Mkaguzi aende akakague hesabu za Serikali kwa sababu hii ni fedha ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuwa katika Muswada huu haionekani wakati gani itafika tupate kura ya maoni. Hamna muda, *timeframe* hamna. Kwa hiyo, nashauri muda ujulikane ili Watanzania tujue tunakwenda vipi kwa sababu naona hamna maelezo hayo kwa kweli.

Mheshimiwa Spika, nikirejea nyuma ni kuwa Watanzania kwa kweli tumeamua tuingie katika mchakato huu kwa usalama kabisa. Kwa hivyo, si vyema likatokea kundi kwa kweli likaanza kuonyesha ishara ya kuleta fujo, hili halitosaidia. Wananchi wanataka Katiba Mpya na Katiba Mpya huwezi ukaipata mahali pengine popote isipokuwa uanze na mchakato huu. Kwa hiyo, ninawaambia wananchi wa Mkoani, Jimboni kwangu ambao kwa niaba yao niko hapa na wananchi wa Pemba, Zanzibar na kwa ujumla Tanzania kuwa hiki tunachokifanya sasa kama ambavyo wamezungumza wenzangu hatutungi Katiba hapa isipokuwa tunaunda vyombo, mchakato, utaratibu wa kuweza kuwafikia wananchi ili kuwaeleza au kupata maoni yao kuhusiana na Katiba Mpya. Kwa hivyo, wakae tayari wakati ukifika waweze kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola simuoni, nimwite Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla simuoni, nimwite Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o simuoni, nimwite Mheshimiwa Rashid Abdallah, ulikuwa unauliza kama umo kwenye orodha, ndio umo sasa, sijui anayekimbia nani?

(*Hapa Mheshimiwa Rashid Abdallah alikuwa akikimbia kurudia sehemu yake illi aweze kutoa mchango wake*)

SPIKA: Nilimwandikia mimi kwamba nina wasiwasи hufikiwi kumbe ndio nimemchanganya. Haya Mheshimiwa Rashid Abdallah, halafu Mheshimiwa Salum Barwany na Mheshimiwa Clara Mwatuka wajiandae.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza sina budi kuchukua nafasi hii kwa kuwashukuru Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Wataalam wake wote. Lakini pia sina budi nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wataalam wake. Pia niishukuru Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kazi kubwa walioifanya katika mchakato wa Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimewashukuru Waziri wa Katiba na Sheria wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Waziri wa Sheria wa Zanzibar kwa sababu kuu. Hawa ni wawakilishi wa Serikali zetu mbili. Walikuwa na wataalam wao kutoka Bara na wataalam wao kutoka Zanzibar. Yaliyofikiwa na wataalam hawa ndio kauli ya Serikali zote mbili.

Mheshimiwa Spika, ni vyema nieleze kidogo, kuna Waheshimiwa katika kujadili pamoja na kwamba ni haki yao, walitoa mawazo yao ni vizuri, lakini walikuwa wanahoji uwakilishi ulio sawa kwa pande zote mbili za Muungano, kwa nini Zanzibar inawakilishwa sawa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hili si suala zuri la kujenga hoja kwa sababu Zanzibar ni sehemu ya Muungano. Ni sawasawa na kuwa na mkataba, kama mtu ni sehemu katika Muungano unamwambia kwa nini mtu yule anakuwepo pale, haileti picha nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano ukienda Ibara ya 127 ya Katiba yetu, Mahakama ni chombo kikubwa kuliko hata hii Tume. Kinasema kwamba Mahakama Maalum ya Katiba itakuwa na Wajumbe amba ni nusu ya jumla ya Wajumbe wote watakaoteuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nusu nyininge ya jumla yote ya wateuliwa kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Hii ni Mahakama ya Katiba, lakini imejali Wajumbe kutoka Zanzibar nusu yake na Wajumbe kutoka Jamhuri ya Muungano nusu yake. Sasa leo mtu anajadili kwa nini Wajumbe wa Tume wanatoka nusu Zanzibar wakati misingi ya Muswada huu ni Katiba yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa pengine anakwenda kuhoji katika kifungu kile cha mamlaka ya Rais. Samahani Mheshimiwa, Muswada wangu kidogo nilikuwa sijajiweka vizuri, nilikuwa nimeondoka.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 9(2), Tume itazingatia misingi mikuu ya Taifa na maadili ya jamii na kwa mantiki hiyo kuhifadhi, kudumisha mambo yafuatayo kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano. Ukitaka kusema kwamba Zanzibar isiwe sawa ni kusema kwamba unapinga Ibara hiyo ya kuhifadhi na kudumisha kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, nachotaka kukisema hapa, Mheshimiwa Waziri mmekaa pamoja na Waziri mwenzako wa Zanzibar na mmekubaliana, haya ndio maamuzi ya Serikali zote mbili na hekima hapa ni nini? Hekima kubwa hapa huu Muswada tusiuchukulie kama Muswada, lakini sawasawa na makubaliano, ni kama mkataba. Serikali ya Zanzibar imesema nini, Jamhuri ya Muungano imesema nini, kwa hivyo sisi Wabunge tuwe na hekima katika kulijadili suala hili kwamba tukirudi nyuma huko kidogo *tuta-create problems*. Wamepewa wataalam wetu, tunawaamini wa pande zote mbili, Kamati ya Katiba na Sheria imekaa, tumejadili kifungu kwa kifungu na nashukuru Mawaziri walikuwa *flexible*, tunawashauri, wanakubali mawazo yetu, wanayaingiza illi twende pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunapojadili hapa ukianza kuleta hoja ya kwamba kwa nini sehemu moja ni kubwa na sehemu moja ni ndogo au kwa nini tuwe sawasawa, utakuwa unaharibu dhana nzima ya Serikali zetu hizi. Kwa maana hiyo, ikija ikitokea mabadiliko haya yakienda kinyume na matakwa ya Zanzibar au kinyume na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lengo la kubadilisha Katiba halitofanikiwa. Nataka Waziri wa Katiba na Sheria na Wabunge wenzangu waangalie kwa makini suala hilo.

Mheshimiwa Spika, pia kuna Wabunge wengine walihoji msingi wa theluthi mbili unatoka wapi, tena ni Waheshimiwa Wabunge nasikitika sana, hebu warejee kifungu 98(1)(b) wataona misingi hasa ya theluthi mbili inatoka wapi. Kwa hiyo, hakuna haja ya kuhoji hayo, kama unataka kuhoji ondoa Katiba iliyopo ndipo unaweza kuhoji mambo haya. Lakini hapa sio wakati wake, tuwaacie wananchi huko wao ndio watahoji na wewe utapewa fursa kwenda kutoa maoni yako huko katika mchakato wa kuchukua kura za maoni.

Mheshimiwa Spika, niende mbele kidogo katika kifungu cha 7(2) juu ya uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti. Kifungu hiki nilipendekeza uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti ufanywe na Wajumbe wenyewe. Halafu kinaendelea kusema Makamu Mwenyekiti atatoka sehemu moja ya Muungano na Mwenyekiti atoke sehemu nyingine ya Muungano, hiyo ikae hivyo.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye kifungu cha 9(1)(a), kazi za Tume. Kazi za Tume ni kuratibu na kukusanya maoni ya wananchi. Mimi nashauri kwa Mheshimiwa Waziri kwamba wananchi wa Tanzania wamo ndani ya Tanzania na wako ambao wako nje ya Tanzania na wapo wengi sana nje, sijui hawa wananchi ambao wako nje ya Tanzania watapata vipi haki hii na kuweza kutoa maoni kwa Muswada huu au kupiga kura za maoni. Kuna nchi mbalimbali zinawafuata wananchi wao katika Mataifa mbalimbali kutumia Balozi zao. Sijui Mheshimiwa Waziri hili ataliangalia vipi. Ni vizuri kuwepo na kifungu kama hicho ili wananchi wote wa Tanzania wapate haki ya kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Spika, macho ya ulmwengu wanaangalia Tanzania, ni namna gani wataendesha mchakato huo, wametulia wanaangalia. Nachotaka kushauri ni kwamba tuwe makini, hili ni suala kubwa lakini sio kubwa nadhani kama tukitulia ni suala dogo tu, ni suala la *place* demokrasia, watu wako huru, tukamaliza kazi. Lakini sasa watu wamelifanya limekuwa jambo kubwa kwa kulikuza yaani kila sehemu ya Tanzania limejaa, limekosa nafasi. Kwa sababu kwa mujibu wa Katiba ni masuala tumekaa, kila mmoja anajua wajibu wake, kila mmoja kutimiza wajibu wake katika nafasi yake. Kwa hiyo, ulmwengu unatuangalia tutafanya nini hasa ukiangalia nchi zetu za jirani za Kenya na nyingine. Nachoomba tuzingatie hizi tofauti ndogondogo baina ya pande zetu hizi mbili tusije tukazibabaisha, tukianza kuzibabaisha, tutaanza mchakato mwininge wa kuja kufanya mazungumzo. Mheshimiwa Waziri angalia kwa makini suala hili, tunaheshimu michango ya Waheshimiwa Wabunge na michango ya wadau, michango ya wanaharakati lakini mustakabali wa makubaliano baina ya nchi mbili hizi lazima upewe nafasi yake kubwa. Ukitosea kutomwamini au kutomfuata Waziri wa Sheria na Katiba kutoka Zanzibar na ujumbe wake ni kusema kwamba maoni ya Serikali ya Zanzibar yote pale umeyaondoa. Nini matokeo yake? Matokeo yake ni kuanza mjadala mpya. Kwa hiyo, wale wanaojadili na kupeleka hizi *schedule of amendments* wawe na uangalifu mkubwa sana kwa maslahi ya Muswada wetu huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, niongeze nyama kidogo kifungu cha 14(1) kuhusu gharama alizozitaja mwenzangu hizi za Tume. Serikali inatumia fedha nyingi sana katika mchakato huo. Ni vizuri wananchi nao wajiridhishe fedha hizi zimetumika kwa lengo liliokusudiwa na ili kujiridhisha ni lazima Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali naye baadaye alete hesabu zake pamoja na kwamba kuna Kanuni za Fedha zinadhibiti masuala hayo, lakini pia ni vizuri tungeona na kama kifungu hiki kingewekwa basi wale ambaowalikuwa na nia mbaya wanaweza wakanusuru matumizi ambayo siyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, nashukuru na naunga mkono hoja, ahsante sana.
(Makof)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Barwany hayupo, Mheshimiwa Clara Mwatuka atafuatiwa na Mheshimiwa Sylvester Mabumba.

MHE. CLARA D. MWATUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami walau nizungumzie machache ili niweze kushiriki katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii leo kuwepo hapa na kunipa uwezo wa kuweza kusimama, ni mapenzi yake.

Mheshimiwa Spika, pia nimshukuru Rais, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kukubali maombi yetu Wana-CUF ambao tuliandamana kuomba Katiba hii. Kwa kweli ni shukrani za pekee, Mungu ampe afya njema, hekima na busara kama anavyofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sitakuwa na mengi ya kusema isipokuwa tu machache ambayo pengine itakuwa kama kutoa ushauri kwa wenzangu, kwa sababu naona kila siku hapa tunapokutana mengi ni malumbano. Tunaacha kile ambacho kimekusudiwa na kujali kwa kuangalia yule amesema nini, inasemekana kwamba mtu ukimjua hakusumbui. Sasa sisi hapa tunafanya kazi ya kumwangalia yule ambaye anaweka akili zetu kwa namna gani, kuzipotosha au kutuchanganya na kuacha lile ambalo tumekusudia. Ndugu zangu naomba tuachane na hilo, wale walio nje...

SPIKA: Kama vile mimi nimeshawajua hamnisumbui. (*Kicheko*)

MHE. CLARA D. MWATUKA: Wale walituleta hapa wanategemea kutusikia tunawatetea wao kwa yale walijotutuma tuje kuyafanya. Sasa tumefikia mahali tumeptoshwa Bunge zima hili badala ya kujadili mabadiliko ya Katiba, tumekwenda kuwajadili hao, kwa kweli nasikitika kwamba hali imekuwa sio nzuri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niombe kwamba katika yale wanayoyasema upande huo, kuna mengi wanayoyasema lakini baadhi yake yanakuwa mazuri na ambayo yangefaa yatumike au yaunganishwe na yale mazuri ya walio wengi. Sasa tusipuuze tu kila jambo kwamba wanasema hao, lakini kwa namna moja au nyininge nisikitike kwamba hao ndio wanapotosha na kuweka kwamba kila wanachosema ionekane hakina maana wakati kina maana.

Mheshimiwa Spika, inavyofahamika katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sehemu ya Pili katika Ibara ya 8(1) ambayo inasema, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayo, samahani macho yenyewe ndio kama hivyo, inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii na kwa hiyo Ibara hii inasema wananchi ndio wenyewe mamlaka yote na Serikali inapata mamlaka na madaraka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii. Fasili ya (b) inasema, sasa lengo la Serikali linakuwa ni ustawi wa wananchi. Halafu (c) inasema, Serikali itawajibika kwa wananchi. Fasili ya (d) inasema, wananchi watashiriki katika shughuli za Serikali yao kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii. Hivyo hapo nisingeona sababu ya wenzangu kuweka malumbano au kupinga kwa sababu leo kama inavyofahamika hatutungi Katiba hapa, tunatoa utaratibu wa kuwapata pengine wale watakaoshiriki katika mchakato wa kukusanya taarifa na kuunda Tume ambayo itafanya kazi hii na sio kwamba tunatunga Katiba leo. Hii kazi itafanywa na wananchi wenyewe ambao ndio wenyewe kauli ya mwisho, hivyo isiwe sababu watu tukaona kwamba tuache kwenda na hilo tukabaki tunalumbana.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nimefurahishwa, wakati tulipokuwa tunadai Katiba nilidhani Mheshimiwa Rais atakataa; ataona kwamba kwa kuwa wanaodai ni Wapinzani lakini hakujali hilo kama alivyofanya Hayati Nyerere kwamba tulipokuwa tunaanzisha Mfumo wa Vyama Vingi yeye akaona kwamba hata hao wachache ndio walioona mbali na ndio watakaoleta mabadiliko ya nchi hii. Wasomi wapo na ndio walioona kwamba ni vyema tuwe na Mfumo wa Vyama Vingi. Sasa hata kwa hili, ndio maana ameona kwamba pamoja na kudaiwa na Wapinzani lakini ukweli upo palepale kwamba kinachotakiwa ni cha msingi. Maana Katiba iliyopo ni ile ya mzazi akiwa na mtoto wake wa kike ambaye hana mjomba wala hana kaka angeweza kujilia mayai mwenyewe. Sasa huyu akaona niondoe hili na nitoe uhuru kwa watu watunge Katiba itakayoendana na wakati.

Mheshimiwa Spika, hilo ndilo ambalo kwa kweli nashukuru na sina sababu yoyote ya kukwepa na kujitenga na Muswada huu kwa sababu matakwa niliyokuwa nayataka yamekubalika, ni moja kwa moja naunga mkono hoja na si mkono mmoja, yote pamoja miguu kwa jinsi nilivyofurahishwa na kitu hiki. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wananchi wenzangu huko nje tukae katika hali ya kupokea Muswada huu na kwamba tutapewa nafasi ya kutoa mapendekezo na mawazo yetu sasa wakati huo ndiyo mzuri na watu wasipuuze, washiriki katika kutoa mawazo yao. Nachoomba Serikali kama kweli tumekuwa na nia kwamba Katiba iwe Mpya basi iwe Katiba Mpya ambayo haiegemei upande wowote. Kwa sababu leo tunasema Chama Tawala ni CCM na hii wala si ya Chama, itungwe Katiba itakayokuwa ni ya kudumu. Maana nchi mbalimbali hivi sasa inaonekana Wapinzani wanachukua utawala, sasa kesho inaweza ikawa hivyo. Sasa kama tukisema tuelekeze upande mmoja, kesho Mungu akipindisha kwa namna nyingine itakuwa ni kilio na majuto. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, twende pamoja, tuunge mkono utaratibu huu ili ije ipatikane Katiba itakayotusaidia sisi wote na naamini tukiwa na nia hiyo moja, Mwenyezi Mungu nafikiri atasema kweli wanangu wameamua na kushirikiana kuwa kitu kimoja na ataibariki. Kikubwa ni kwamba wote Waislam au Wakristo tunapokwenda Misikitini na Makansani tuwe tunaomba tupate Katiba ambayo itakuwa ni Katiba ya nchi tukiamini kwamba Katiba hiyo ndiyo itakayoendelea kwa miaka mungi huko mbele kwa sababu si kitu kinachopatikana kila mwaka. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawaomba wenzangu tushirikiane kwa nia moja, tukipendana na kuona kwamba mawazo watakayotoa hata wale wanyonge kule vijijini ni mawazo ya kweli ili mradi yaonekane kwamba yanafaa. Tutakapofanya hivyo, ndipo Utaifa utakapoonekana kwamba sisi ni ndugu bila kujali kwamba kuna Uzanzibar na Ubara. La nini kama wote tumeungana? Nchi yetu ni moja, sasa tunapobaguana sio vizuri. Baba yetu ni mmoja, Mheshimiwa Kikwete, hatuna Rais mwingine hapa. Mimi niliyesimama hapa ambaye sikumchagua kulingana na kwamba kulikuwa na mgombea wangu ambaye nilimpendekeza kwamba angekuwa Rais, aliposhindwa mimi ni wa Kikwete. Ni sawasawa na iliyokuwa Jimboni kwangu pamoja na kugombea, mimi nikakosa nafasi akapata ndugu yangu Mama Kasembe na yeye ni Mbunge wangu wa Jimbo langu, sibagui. Kwa hiyo, hali iliyopo ni sisi kupendana na kushirikiana na kuheshimiana. Anachosema yule ilimradi kiwe cha maana tukifuate. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nafurahia sana mpango huu. Ila niongeze moja la elimu, ule utaratibu wa kusema watoto waanze shule wakiwa na umri wa miaka sita, kwa kweli hawa watamaliza wakiwa wadogo. Tunaona wenyewe ndani humu, Wabunge wengine wadogo hata heshima au hadhi ya Bunge inapungua. (*Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Mwatuka, hilo halimo kwenye Katiba.

MHE. CLARA D. MWATUKA: Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba ingeendelea ile ile miaka saba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mpaka hivi sasa nishukuru kwa yote ambayo yameamuliwa hapa na kwa wale ambao wamechangia yale ambayo yamehitajika hapa basi nawapongeza na Mungu azidi kuwapa afya njema na wengine wachaguliwe wawepo kwenye Tume hiyo ili wakatuandalie vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naunga mkono hoja tena mia kwa mia. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Kwa mapendekezo ya Sheria hii, Wabunge hamtakuwa kwenye Tume hiyo wala Baraza la Wawakilishi hawatakuwemo, mtakuwa labda kwenye Bunge Maalum lakini sio Tume. Sasa namwita Mheshimiwa Sylvester Mabumba.

MHE. SYLVESTER MASSELLE MABUMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nipate nami kutoa mchango wangu katika mjadala huu wa mabadiliko ya Sheria ya Katiba ya mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda sana kutoa pongezi zangu kwa Serikali yetu, kwa umakini wake, kwa mapenzi yake kwa Watanzania, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kuona umuhimu baada ya miaka 50 kuititia upya Katiba yetu ili kuangalia kama inafaa kuendelea kuongoza Taifa letu au tuje na Katiba nyingine ambayo baada ya miaka 50 itaweza kuongoza nchi hii ili kuwa na mustakabali mzuri wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba Tanzania kwa mara nyingine inaonyesha ulimwengu kwamba ni nchi ya kidemokrasia. Ushirikishwaji wa Bunge hili kujadili namna ya kuunda Tume ambayo itapitia ukusanyaji wa maoni ya wananchi kuyachambua na kuyaratibu, ni dalili njema kwamba nchi hii imejengwa katika misingi ya kidemokrasia na si ya kidikteta kama wengine wanavyodai. Katika nchi ambazo ni za kiimla, yaani za kidikteta, inaweza ikaundwa timu ya watu wachache sana ambayo itazingatia maslahi ya walioko madarakani lakini Tanzania si nchi ya mfano huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nielekeze mchango wangu kwenye Muswada wenye nianziazia na Sehemu ya Tatu ya Muswada huu ambayo inazungumzia uundwaji wa Tume.

Mheshimiwa Spika, kwenye Ibara ya 6(3), napongeza sana maoni ambayo yamewekwa hapa kwamba Wajumbe wa Tume watakuwa *vetted*. Pamoja na sifa ambazo zimewekwa hapa lakini tuangalie sana uzalendo wao juu ya kuulinda Muungano wetu. Pamoja na kuwa na *background* ya kuwa na mambo ya Katiba, mambo ya Sheria na nini lakini sifa ya ziada iwe ni kuangalia uzalendo wao.

Mheshimiwa Spika, pia naunga mkono sana Ibara ya 9 ambayo inaelezea majukumu ya Tume. Kazi ambazo zimeelezwa hapa kwa maoni yangu zinatosheleza sana kwa nyongeza ya sehemu ya Ibara ya 16 kwamba Kamati hiyo au Tume hiyo itaweza kufanya kazi vizuri. Sifa ambazo zimewekwa pale zinaonyesha dhahiri kwamba kama zitazingatiwa, Tume itaweza kweli kukusanya maoni kwa uhuru bila kuingiliwa, kuyachambua na kuzingatia michango ambayo wananchi watakuwa wameitoa. Kwa hiyo, kwa maoni yangu, naomba basi kama kuna hadidu rejea basi Ibara ya 9 na ya 16 zitakuwa zimekidhi mahitaji hayo.

Mheshimiwa Spika, nikiendelea na mchango, naomba pia nizungumzie kwenye Ibara ya 24 ambayo inazungumzia kuhusu Bunge la Katiba. Kwenye eneo hili naunga mkono sana kwamba Bunge hili, naomba kunukuu: "*Bunge la Katiba linaweza kuanda Kanuni kwa ajili ya kuendesha shughuli katika Bunge la Katiba.*" Hapa naomba sana litakapokuja kuundwa Bunge hili la Katiba liwe na uhuru kweli wa kuona namna gani linaweza likaendesha shughuli zake. Kwa hiyo, napendekeza ile sehemu ndogo ya Ibara ya 24 inayozungumzia masharti ya Muswada wa Katiba yapate kuitishwa katika Bunge la Katiba itakayohitaji kuungwa mkono na theluthi mbili. Naomba Ibara ndogo hii ingefutwa kabisa ili kulipatia nafasi Bunge lenyewe la Katiba kuja kuangalia utaratibu utakaofaa wakati huo utakapofika. Tunapoiwekea Ibara ndogo ya tatu maana yake tunalipunguzia nguvu za kuandaa utaratibu ambao tunaona unafaa.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie kuhusu uhuru wa Tume za Uchaguzi, Tume ya Uchaguzi ya Taifa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Naomba pia katika eneo hili madaftari ya kudumu, naamini yaliandaliwa kwa ustaarabu na kwa ustadi kwa kuzingatia kanuni na taratibu zilizopo. Kwa hiyo, naomba tuwe na imani na Tume hizi mbili. Maoni ya kwamba zawenza kuchakachua maoni ya wananchi, hii ni hatari. Ni hatari kwa sababu Tume hizi zinaongozwa na Majaji ambao wanaviapo vyao, haki zetu zote tunazipata kwenye Mahakama na Mahakama zinaongozwa na Majaji. Sasa tuwe na Majaji ambao wanaongoza Tume hizi. Hatuna mtu anayeongoza Tume ambaye sio Jaji. Tukiangalia Tume ya Taifa ya Uchaguzi inaongozwa na Mwenyekiti ambaye ana-*background* ya Sheria na amewahi kuwa Jaji na tukiangalia kule Zanzibar Mwenyekiti wa Tume ana-*background* ya Sheria. Wanasheria wanamiliko na viapo, ni

sawa na Wachungaji na Masheikh. Sasa kama mtu anafika wakati hana imani na Sheikh au Mchungaji au Padri, huyo ni hatari sana.

Mheshimiwa Spika, tunavyoamini sisi kwenye imani zetu, viongozi hawa ni wapakwa mafuta na Majaji kwa sababu ni watoa haki kwa vyovyote vile hawatakuwa na muda wa kuchakachua maoni ambayo yatakuwa yamejazwa mashabiki ya Chama kimoja cha CCM, ni majina ya Watanzania wote na hata tumeona tulipoenda kwenye uchaguzi mwaka jana walikuwa huru kuchagua kiongozi wanayemhitaji na kwa bahati njema sana mwaka jana waliipatia ridhaa CCM chini ya kiongozi wetu mpendwa Jakaya Mrisho Kikwete. Kwa hiyo, hakuna ushabiki hapa na hata kule Zanzibar daftari ile ndilo ambalo lilitumika kwenye uchaguzi na wananchi wa Zanzibar wakaipatia ridhaa CCM. Leo Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein ndiye kiongozi wetu mkuu na kwa ustaarabu mkubwa alikubali kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa upande wa Zanzibar ili kuimarisha umoja na mshikamano. Sasa kwamba madaftari yatachakachuliwa sioni mantiki yake. Naomba sana tuwe na imani na kwa vile mengi sana yamesemwa nisingependa kurudia yale ambayo yamesemwa na wenzangu.

Mheshimiwa Spika, kwa mchango wangu huu mdogo, naomba sana niwe mmoja kati ya ambao wameshiriki kuchangia mabadiliko ya Muswada wa Katiba wa Mwaka 2011. Nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MHE. ZAHRA ALI HAMAD: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia na mimi japo machache katika Muswada huu muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nianze kwa kukushukuru wewe binafsi kwa ushirikiano mkubwa ambao ilitupa katika Kamati yetu ya Katiba na Sheria, kila ambapo ilituona tunakwama, ijapokuwa ni wajibu wako kama Spika wetu lakini uungwana mtu akifanya jambo zuri basi ni kumwambia ahsante, tunakushukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pili nimshukuru Mwenyekiti wetu wa Kamati, kwa uvumilivu mkubwa ambao aliuonyesha na huu kwa kweli ni ukomavu wa kisiasa kwa sababu Muswada huu hakuwa mwelesi sana katika Kamati yetu. Niwashukuru Mawaziri wote wawili, yule wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Celina Kombani na Mheshimiwa Abubakar, Waziri wa Katiba na Sheria wa Zanzibar na haya ni matunda ya ile Serikali ya pamoja *GNU*, ni Waziri ambaye anatoka katika Chama change, namshukuru sana pamoja na Watendaji wao wote wa Zanzibar pamoja na Bara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi kwa vile nilishiriki katika Kamati, nisingekuwa na mengi sana ya kuzungumza lakini nina machache sana ya hapa na pale. Nataka niwaombe Wabunge wenzangu, naheshimu sana mawazo yao, naheshimu sana mapendekezo yao lakini katika ile Ibara ya 6(2), naomba tubakize kama ilivyo. Kwa sababu haya ni matakwa ya Katiba ambayo tunakwendanayo mpaka hilvi sasa. Lakini pili ni makubaliano ya dhati ambayo yalifikiwa na Serikali zetu mbili. Lakini tuone pia kama tutaiondoa Ibara hii kama ilivyoletwa hapa Bungeni, tutaweza kurudisha malumbano yale ya mwanzo ambayo si vizuri kwa hatua hii ambayo tumefikia basi tukarudi kule nyuma ambako tulikokuwa.

SPIKA: Ibara inasemaje?

MHE. ZAHRA ALI HAMAD: Mheshimiwa Spika, ni ile ambayo inasema theluthi mbili kati ya Zanzibar na Bara katika upigaji kura.

Mheshimiwa Spika, pia nataka nikubaliane na kifungu cha 30 kinachozungumzia juu ya kutumia Daftari la Wapigakura la Kudumu la Zanzibar, sina tatizo na hilo lakini niombe Serikali zetu zihakikishe Watanzania wote wanapata haki yao ya kupigakura. Bado madaftari hayo japo ndiyo yalituleta hapa na hata mimi nimepita huko mpaka nikafika hapa lakini bado lina matatizo na kuna Watanzania wengi ambao wanakosa haki yao ya Kikatiba hususani Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, pia kwenye kifungu cha 20, pametajwa pale Wabunge ambao watashiriki katika Bunge la Kutunga Katiba. Mimi sina tatizo na hilo, isipokuwa naomba tu, kuna taasisi zile ambazo zimetajwa katika ile 116, basi ni vizuri hasa zile zinazozungumzia Vyama vya Siasa, kuwe na mawasiliano ya Rais na viongozi wa Vyama hivyo. Mfano mzuri tunao sisi Wazanzibari, Rais huwa anateua Wawakilishi kuingia Barazani kupitia Upinzani lakini kwa mashauriano makubwa na viongozi wa Vyama hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikitoka huko kwenye Muswada, nilitaka kidogo nizungumze na Wabunge wenzangu. Kiongozi ni yule anayeonyesha njia. Sisi tuko hapa kuonyesha njia kwa wale wananchi wetu ambao wametuleta. Inawezekana ukaonyesha njia ya kuweza kufika haraka pale ambapo wananchi wanalenga wafike lakini si vizuri kuweza kutumia fursa hii ambayo wenzetu wameona tutawakilisha, tukaanza sisi kuwa cheche ambayo hatma yake inaweza ikafanya moto mkubwa na tukashindwa kuuzima katika kipindi hiki ambacho tunacho.

Mheshimiwa Spika, katika hilo, nataka niwanukuu viongozi wawili. Kuna kiongozi mmoja alisema, mdomo ni nyumba ya maneno na ulimi ni mdogo na ni laini sana, lakini Mwenyezi Mungu kwa sababu anajua madhara ya ulimi, aliuhifadhi, akaujengea geti - yaani haya meno ambayo tunayo. Lakini unapotoka na kutoa kauli, kauli ambayo inatoka ni mshale ambao unaweza ukaumiza umma. Sasa ikiwa ni mshale ambao unaumiza, utizame sumu yake inakuwa ni sumu ya kiasi gani. Pia akasema, namshukuru Mwenyezi Mungu, ulimi ni mfupi laiti ulimi ungekuwa mrefu ukaweza kufika kwenye goti la mguu, basi nadhani Dunia isingekuwepo. Huyo ni Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha aliyekuwa Waziri Kiongozi wa Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuna kiongozi mwagine pia alisema hajawahi kumwona mtu kujuta kwa kunya maza, ameona watu wengi wakijuta kwa kusema. Tusijekuwa mionganoni mwa wenyewe kujuata kwa kusema, tukaja tukajitea nchi mtafaruku mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi namshangaa sana ndugu yangu Tundu Lissu na *walaah* sikuwa na haja ya kumtaja, lakini kwa sababu kanitaja, basi na mimi ni lazima nimirage.

Mheshimiwa Spika, naomba nimnukuu Mheshimiwa Tundu na *walaah* Mheshimiwa Marehemu Babu yangu aliniambia kwamba jina zuri ni dawa kwa mtoto, umpe mtoto jina zuri ili maisha yake yawe mazuri. Unapompa mtoto jina bayaa basi hatma yake inakuwa mbaya hata kama umemsomesha kiasi gani. Hili Tundu tunaweza tukajua jina, lakini mimi Lissu kwa Wazanzibari siwezi kukwambia Mheshimiwa Spika, siwezi kusema ndani ya Bunge lako hili Tukufu na kwa maadili yetu, naliacha kama liliyvo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ni pale aliposema kuwa, naomba kunukuu:-

"Mapendekezo haya yanaashiria kuwepo kwa mtazamo ambapo chanzo chake ni makubaliano ya Muungano kati ya Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Jamhuri ya Tanganyika ya tarehe 25 Aprili, 1964. Kwa mtazamo huu, inaonekana Zanzibar ni nchi hulu".

Mheshimiwa Spika, Zanzibar ni nchi hulu ambayo ina Rais wake na bendera yake. Zanzibar ina Baraza la Wawakilishi ambalo linatunga Sheria, Zanzibar ina Rais na Mawaziri ambapo mimi ni mionganoni mwa Mawaziri wanaotoka Zanzibar na Zanzibar haijawahi kuwa koloni la Bara, haitakuwa, itaendelea kuwepo, labda Wazanzibari wote tufe kwa pamoja, Mungu atunusuru, kama vile ambavyo Bara haijawahi kuwa koloni la Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa huyu aliendelea kusema kuwa, naomba kumnuukuu:-

"Pili, kuna dhana potofu kuwa Rais wa Zanzibar hakushirikishwa katika mchakato wa maandalizi ya Muswada wa zamani". Dhana hii ni potofu".

Mheshimiwa Spika, viongozi...

(*Hapa kengele illilia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji*)

MHE. ZAHRA ALI HAMAD: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja! (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante! Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zina-cut across. Kwa hiyo, hata kama mngependa kumkopesha muda wenu, hamna nafasi hiyo. Sasa, ukiangalia mazungumzo tunayoendelea nayo, bado orodha ni ndefu sana, lakini kwa mamlaka niliyonayo...

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mwongozo wa Spika!

SPIKA: Ninaposimama mimi huwezi kunipa mwongozo! Naomba ukae! Tunaendelea. Ninasema kwa jinsi tunavyofuatilia mazungumzo katika siku chache tulizozungumza, ukiangalia wote mnarudia tu, hakuna jipya kabisa. Sasa, mimi ningependa tutoe nafasi kwa wanaoandaa majibu kusudi kesho asubuhi tuweze kupata majibu yaliyo sahihi, yenyé kina. Kwa sababu huu Muswada pamoja na kwamba ni sheria ya kawaida tu ya kuunda Tume ili ianze kazi ya kukusanya maoni, lakini ni Muswada ambao tungependa ukae vizuri. Kwa hiyo, tunapenda hao watakaohusika kujibu hoja mbalimbali, wazijibu vizuri. Kwa hiyo, kesho asubuhi tunaweza kuendelea nao. Haya Mwongozo wa Spika!

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68. Gazeti la leo la Tanzania Daima, limemdhaliisha Spika wetu kwa kuandika taarifa ambayo siyo sahihi. Kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge, Mbunge ye yote anaweza akaingia kwenye Kamati yoyote, lakini humu ndani imeandikwa kwamba wewe unatulazimisha sisi tuingie kwenye Kamati, jambo ambalo siyo la kweli. Ninaomba mwongozo wako. (*Makofi*)

SPIKA: Kama kawaida magazeti mengine yana kazi ya kupotosha ukweli na kuandika yale wanayotamani wao. Kama Spika, naweza kuagiza kazi fulani iende kwenye Kamati yoyote ile wakati wowote ule. Hivi sasa kuna *amendments* ambazo Wabunge wameleta, mimi ningependa sana wakapate muda mzuri sana kwenye Kamati wakazungumze. Hiyo haina maana kwamba walioleta *amendments* hawataruhusiwa kuingiza *amendments* zao hapa. Lakini tulitaka wapate upana zaidi kuliko sisi kubishana humu, inakuwa siyo vizuri. Watarudisha *amendments* zao humu ndani, lakini waende wakakae na Kamati na Wizara wakazijadili vizuri zaidi. Kwa hiyo, kazi ya Spika ni pana, simlazimishi mtu, ndiyo madaraka niliyopewa kwa mujibu wa Kanuni zetu na Katiba. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kwa sababu zile nilizosema kwamba tungependa sana wenzenetu wapate muda wa kutosha kuweza kuzipitia zile hoja mbalimbali zilizotolewa hapa na Watanzania waweze kupata ukweli wa kila kitu kilichowekwa hapa. Ni sheria ya kuwezesha kuanzisha mchakato wa kuingia kuandika Katiba. Madaraka ya Rais yapo kwenye Katiba hii, kwa hiyo Muswada wetu huu hauwezi kumwondolea Rais madaraka. Huu ni Muswada mdogo sana ukilinganisha na Katiba tuliyonayo. Kwa hiyo, Muswada mdogo tu hauwezi kumwondolea Rais madaraka yake kwenye Katiba jamani! (*Makofi*)

Nafurahi sana tuna wasomi wetu hapa leo, wengine asubuhi niliwataja, nadhani walikuwa wamekosa nafasi. Tulikuwa na wanafunzi 72 kutoka Chuo cha Biashara *Campus* ya Mwanza na ya Dar es salaam, halafu na viongozi 8 wa wanafunzi kutoka matawi yote matatu, Chuo cha Dar es salaam, Dodoma na Mwanza. Kama wapo, naomba wasimame tuwatambue. Ahsanteni sana na karibuni sana. (*Makofi*)

Katika ofisi zenu, hii Miswada mnaweza kuipata na mnaweza ku-download pia katika website ya Bunge. Tunaomba sana ninyi wanafunzi msome haya mambo kwa umakini sana. Tunachokifanya hiki ni kwa manufaa yenu, wala siyo vinginevyo. Kwa hiyo, msome objectively, siyo hii kusikiliza mtu kwa sababu ana siasa zake, basi siyo vizuri. Ahsanteni sana kwa kuja, karibuni tena. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tutaahirisha kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 6.50 mchana Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,
Tarehe 18 Novemba, 2011 Saa Tatu Asubuhi)*